
SportPesa
TZS. 1,119,012,860
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Kizimbani** madai kusambaza picha video za Profesa Jay UK. 3





# Nipashe

Jumatano Aprili 6, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580907

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

igital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US




# MAUMIVU

• **Bei** mafuta ya petroli, dizeli zapaa, TABOA yajipanga kupandisha nauli, bidhaa nazo... *Endelea ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na viongozi wa vyama vya siasa, mabalozi, wawakilishi wa taasisi mbalimbali, wakati akifungua mkutano wa Haki, Amani na Maridhiano, ulioandaliwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), jijini Dodoma jana. Kulia ni Mwenyekiti wa TCD, Zitto Kabwe na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana. **PICHA: IKULU**

## Samia aziweka mtegoni TCD na kikosi kazi

UKURASA 3

## Wabunge wataka kamati huru uchafuzi Mto Mara

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA SASA AKILI ZOTE LIGI KUU** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula (kulia), akizungumza katika kikao cha kujadili mgogoro wa ardhi katika makazi ya wazee wasiojiweza ya Nunge, Kigamboni, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwakilishi wa Wizara ya Katiba na Sheria, Aman Manyaga na Mwakilishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Nuru Julius. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Maumivu kupanda bei za petroli, dizeli

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wametoa maoni tofauti kuhusu kupanda kwa bei ya mafuta huku Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), kikieleza kuanza mchakato wa kupandisha nauli kutokana na ongezeko hilo.

Jana, Mkurugenzi wa Petroli wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Gerald Maganga, alisema bei ya mafuta ya petroli itakayoanza kutozwa leo imeongezeka kwa Sh.321 kwa lita sawa na asilimia 12.65, huku dizeli ikiongezeka kwa Sh. 289 na mafuta ya taa kwa Sh. 474 kwa yanayopokelewa kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Akizungumza Nipashe, Mkurugenzi wa Habari wa TABOA, Mustapha Mwalongo, alisema kwa sasa wapo kwenye mchakato wa upandishaji nauli kutokana na ongezeko la bei ya mafuta.

"Tupo katika kufuata hatua za upandishaji wa nauli ambao unatutaka tupeleke mahesabu LATRA (Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini), si chini ya kampuni nne zipeleke mahesabu LATRA kuonyesha ni namna gani tunavyopata hasara."

"Si suala la mafuta tu pia kutakuwa na ongezeko la bei za vipuri na vifaa vingine vinavyohusu sekta ya usafirishaji, tutaainisha vitu vyote tutapeleka mahesabu na tutawaonyesha namna gani kwa sasa tunavyofanya biashara na kupata hasara," alisema.

Alisema maombi ya kupandisha nauli tayari wamepeleka sasa wanapaswa kupeleka hesabu.

"Tukikamilisha hesabu tutakwenda kuwasilisha kwenye mkutano na baada ya hapo tutatembea mikoa minne na watu wa LATRA watatembea mikoa minne kuelezea maombi ya wasafirishaji kupandisha nauli kuuliza mtu mwenye hoja ya msingi ya kuzuia nauli isipande," alisema.

Alisema kuwa mkutano wa mwisho utafanyika jijini Dar es Salaam na mikoa itakayotembelewa ni Mwanza, Kigoma, Mbeya na mingine na baada ya hapo itatolewa hitimisho la kupandisha nauli.

"Ni mchakato mrefu kidogo, lakini tayari tumeshaingia kwenye mchakato," alisema.

Naye Mchambuzi wa masuala ya uchumi kutoka Chuo cha Biashara (CBE), Dk. Nassib Mramba, alisema hali hiyo itasababisha mfumuko wa bei.

"Tutarajie miezi minne mitano bei zitaongezeka za mafuta, athari zitakuwa kubwa na tutarajie mfumuko wa bei mkubwa sana ambao haujawahi kutokea miaka mingi iliyopita," alisema.

Alishauri serikali kuondoa matumizi yasiyo ya lazima ikiwamo mbio za Mwenge ili fedha zitakazookolewa zitumike kupunguza makali ya gharama za mafuta. "Kwenye matumizi ambayo hayana madhara ya moja kwa moja kwa wananchi hayo yaondolewe ili kufidia gharama za mafuta zisiendelee kupaa," alisema.

Kwa upande wake, mwendesha bodaboda Ali Saidi, alisema hawajazoea ongezeko hilo ambalo litasababisha kupanda kwa gharama za maisha hasa ikizingatiwa watu wapo kwenye mfungo wa Ramadhani na Kwaresma.

Kadhalika, Pendo Joseph, mkazi wa Makulu, alisema ipo haja kwa serikali kuangalia unafuu kwa watumiaji kwa kuwa hali hiyo itasababisha bei ya bidhaa nyingine kupanda.

Dereva wa gari, Mussa Gaitan, alisema ongezeko limepanda kwa kiwango kikubwa tofauti na siku za nyuma linapanda kwa kati ya Sh. 50 hadi 60 kwa lita, hali itakayosababisha baadhi ya watu kutoendesha vyombo vyao vya usafiri.

Akitangaza bei ya mafuta jana jijini hapa, Mkurugenzi Maganga, alisema kwa Mkoa wa Dar es Salaam petroli kwa lita itakuwa Sh. 2,861, dizeli ni Sh.2,692 na mafuta ya taa Sh. 2,682 huku kwa Mkoa wa Arusha lita ya petroli ni Sh. 2,905, dizeli Sh.2,836 na mafuta ya taa Sh.2,766.

"Mkoa wa Pwani bei ya petroli kwa lita itakuwa Sh.2,866, dizeli Sh.2,697 na mafuta ya taa Sh. 2,686, Dodoma petroli itakuwa Sh. 2,920, dizeli 2,751 na mafuta ya taa ni Sh. 2,740 kwa lita," alisema.

Kadhalika, Mkoa wa Geita petroli Sh. 3,027, dizeli Sh. 2,858 na mafuta ya taa Sh. 2,847, Iringa petroli Sh.2,926, dizeli 2,756 na Sh.2,746 kwa lita ya mafuta ya taa.

Alisema bei hizo zimechangiwa na ongezeko la bei ya mafuta katika soko la dunia inayotokana na mgongano uliopo wa Urusi na Ukraine na kurejeshwa kwa tozo ya Sh. 100 kwa lita iliyositishwa kuanzia mwezi Desemba 2021 hadi Machi, 2022.

"Mikoa ya Kaskazini yaani Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara, zimeongezeka kwa Sh. 285 kwa petroli na dizeli Sh. 295 kwa lita, mikoa ya Kusini yaani Mtwara, Lindi na Ruvuma zitakuwa Sh. 281 kwa lita ya dizeli," alisema.

Akizungumzia hali ya upatikanaji mafuta nchini, Maganga alisema akiba iliyopo ni ya siku 19.


MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

NOTISI YA KULIPA DENI /TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **FNB Bank Tanzania Limited**, **MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunamtangazia mdaiwa au mteja wa benki tajwa hapo juu kulipa mkopo wake ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili kwenye gazeti. Kushindwa kufanya hivyo kutapelekea sisi kuuza dhamana ya wadaiwa aliyoiweka benki wakati anachukua mkopo kwa njia ya mnada wa hadhara. Mnada utafanyika mahali nyumba/dhamana iliko kama inavyoonesha hapa chini kwenye jedwali.

| S/N | JINA LA MTEJA/MDAIWA | AINA YA DHAMANA | DHAMANA MAHALI ILIKO | TAREHE YA MNADA NA MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | DOTTO JOSEPH IBAMBASI | FIRST CHARGE LEGAL MORTGAGE RESI DENTIAL PROPERTY TITLE NO. 92587, PLOT NO. 15 , BLOCK CC, TABATA KINYEREZI, KISIWANI STRE ET | KISIWANI STREET, KINYEREZI, ILALA MUNICIPALITY | 20/04/2022 SAA: 09 :00 HADI SAA 5:00 ASUBUHI<br>MNADA WA HADHARA |

**Masharti ya mnada**
1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei ya mnada mara baada ya nyundo ya dalali kutua.
2. 75% inayobaki itatakiwa kulipwa ndani ya siku 14.
3. Gharama za kuhamisha umiliki wa dhamana ni za mnunuzi
4. Dhamana itauzwa kama ilivyo

MAWASILIANO
+255 765 999 000 AU +255 623 382 878 AU (+255 627 838 627 MWANZA TU)


# Wabunge wataka kamati huru uchafuzi Mto Mara

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WABUNGE wameikataa ripoti ya Kamati ya Kitaifa iliyochunguza uchafuzi wa Mto Mara mwezi uliopita huku wakiitaka serikali kuunda kamati huru kuchunguza chanzo cha uchafuzi wa mto huo na mustakabali wake.

Vilevile, baadhi wamependekeza kufanyike uchunguzi dhidi ya wajumbe wa kamati ya kitaifa iliyofanya uchunguzi huo, wakidai ripoti yao inaonesha kuwapo shida za kimaadili.

Hayo yaliibuka jana kwenye Ukumbi wa Msekwa bungeni jijini Dodoma wakati wabunge walipokuwa wanajadili ripoti hiyo iliyopowasilishwa na wajumbe wa kamati ya kitaifa walioongozwa na Mwenyekiti, Prof. Samwel Manyele, aliyewahi kuwa Mkemia Mkuu wa Serikali.

Katika kikao mahususi cha kupokea ripoti hiyo, wabunge 18 walipata nafasi ya kuchangia moja kwa moja na wote waliikataa ripoti hiyo na kutaka kuundwe kamati nyingine waliyoiita huru itakayotaja chanzo halisi cha uchafuzi na vifo vya samaki kwenye mto huo.

Hata hivyo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, aliwataka wabunge kuwa makini katika ndimi zao, akiwa na angalizo kwamba kuna mambo mengi yenye maslahi kwa nchi ambayo yakiendewa kwa haraka, madhara yake yatakuwa makubwa.

Dk. Jafo aliwataka wabunge kuisoma ripoti nzima na watakapoanza kuijadili wawe na muda wa kutafakari kwanza maslahi ya nchi na kutanguliza mbele uzalendo.

Neema Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, ndiye alikuwa wa kwanza kuchangia mjadala huo, akiibua hoja tatu ambazo ni pamoja na alichokiita mgongani wa maslahi miongoni mwa wajumbe -- kwamba Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilikuwa na mjumbe ndani ya kamati ilhali lenyewe ni sehemu ya watuhumiwa kwa kushindwa kusimamia mazingira ya Mto Mara.

Alihoji sababu za Wizara ya Afya na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kutokuwa na wajumbe ndani ya kamati ya kitaifa ilhali uchafuzi umeathiri afya za watu na usalama wa chakula (samaki) ambao TBS unawahusu.

"Hoja ya tatu, kwa nini ripoti ya awali ya kamati hii ya kitaifa ilisema samaki wamekufa na kuelea kutokana na kinyesi cha mifugo na sasa inasema wamekufa kutokana na kutibuliwa kwa tope?" alihoji.

Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, alifuatia huku akihoji alichokibaini katika ukurasa wa 46 wa ripoti ya kamati kubainika kuwapo kiwango cha zebaki ndani ya maji ya Mto Mara, lakini kamati hajazungumza chochote kuhusu hilo kwenye matokeo ya uchunguzi wake.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mara, Agnes Marwa, alihoji kile alichokiita kamati kukimbilia kuweka utetezi kwamba Mgodi wa Barrick North Mara hauhusiki na uchafuzi wa Mto Mara.

"Bunge liunde tume huru iende ikachunguze chanzo halisi cha uchafuzi wa Mto Mara.

Wabunge wa maeneo hayo tushirikishwe. Kamati kama hii ya Prof. Manyele ni matumizi mabaya ya fedha za umma, mmetumia hadi ndege za jeshi mnaleta vitu vya aibu," alishauri.

Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, alishauri wajumbe wa kamati ya kitaifa wachunguzwe kutokana na kile alichodai kuonekana shida kwenye uadilifu wao.

"Ripoti tatu zote zinatofautiana. Ile ya Bonde la Ziwa Victoria inasema kuna mafuta na grisi. Ile ya Kisumu, Kenya inasema jambo tofauti. Hii ya Prof. Manyele na wenzake inatumbia kinyesi cha mifugo na top. Tutakwenda kuwaeleza nini wananchi?

"Jambo hili ni kubwa, ni maisha yetu. Leo asilimia 74 ya wagonjwa wa saratani pale (Taasisi ya Saratani) Ocean Road wanatoka Kanda ya Ziwa," alitahadharisha.

Mbunge wa Rorya, Jaffari Chege, alisema kuna haja kuundwa kamati nyingine kuchunguza uchafuzi huo, akidai kuwa baadhi ya vijiji ambavyo vimetajwa kwenye ripoti kwamba wakazi wake walihojiwa na kamati, haviko Rorya.

Kasalali Mageni, Mbunge wa Sumve, akichangia mjadala huo, alisema: "Bunge kabla ya kuunda kamati nyingine, tuichunguze kwanza kamati hii maana imeleta taarifa yenye ualakini mkubwa, imejaa wasomi lakini inazungumza vitu ambavyo hata mtoto mdogo hawezi kuvizungumza."

Machi 12, mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Sulemani Jafo, aliunda kamati hiyo ikiwa na wajumbe 11 kutoka taasisi mbalimbali za serikali, akiipa siku saba kufanya uchunguzi hadi Machi 19, mwaka huu ilipowasilisha ripoti kwake mjini Musoma.

Mbali na Mwenyekiti Prof. Manyele, wajumbe wengine wa kamati hiyo ya kitaifa ni pamoja na: Katibu Dk. Samuel Mafwenga, Mkurugenzi Mkuu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC); Dk. Kessy Kilulya, Mkuu wa Idara ya Kemia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM); Dk. Charles Kasanzu kutoka Idara ya Jiolojia UDSM, Daniel Ndio, Mkurugenzi wa Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA); na Renatus Shinhu, Mkurugenzi Mamlaka ya Bonde la Maji Ziwa Victoria.

Wengine: Baraka Sekadende, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Samaki (TAFIRI) - Mwanza; Dk. Neduvoto Mollel kutoka Mamlaka ya Afya ya Mimea na Usimamizi wa Viatilifu (TPHPA), Ofisa kutoka Ofisi ya Rais Ikulu; Yusuf Gobe Kuwaya kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara na Faraja Ngelageza, Mkurugenzi Msaidizi Bioanuai, Ofisi ya Makamu wa Rais.

Katika taarifa iliyowasilishwa Mjini Musoma, Kamati ilibainisha njia kuu mbili zilizochafua maji ya Mto Mara; mosi kupitia mimea ya asili inayozalisha sumu na pili ni shughuli za kibinadamu ikijumuisha uwapo wa idadi kubwa ya mifugo inayozalisha ziada ya kinyesi katika maji hayo.

HABARI KITAIFA

# Kortini madai ya kusambaza picha ya video ya Profesa Jay

Na Kulwa Mzee

MKURUGENZI wa Mtandao wa Kijamii wa Uturn Collection, Allen Mhina (31), na Mange Kimambi App, wameshtakiwa mahakamani kwa mashtaka matatu likiwamo la kuchapisha maudhui yanayokiuka haki na uhuru wa mtu mwingine.

Washtakiwa hao walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate na kusomewa mashtaka na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mwanaamina Kombakono.

Miongoni mwa mashtaka mengine yanayowakabili ni kufanya kazi ya uandishi wa habari bila kuwa na kibali kutoka bodi ya ithibati ya wanahabari na kumfedhesha mtu kwa njia ya mtandao.

Wakili Kombakono akisaidiana na Sylvia Mitanto, walidai kuwa Machi 9, 2022 katika maeneo tofauti ndani na nje ya Tanzania, washtakiwa walichapisha video ya aliyekuwa Mbunge wa Mikumi, Joseph Haule, maarufu kama Profesa Jay, ambaye amelazwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kitengo cha wagonjwa mahututi (ICU) maudhui ambayo yanadhuru haki ya faragha ya mgonjwa (Profesa Jay).

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa katika tarehe tofauti kati ya Septemba 22, 2021 na Machi 14, 2022, Kinondoni eneo la Manyanya katika Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, mshtakiwa Allen na Kampuni ya Uturn Collection, walifanya kazi ya uandishi wa habari bila kuwa na kibali kutoka bodi ya ithibati ya wanahabari.

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa Machi 9, 2022 katika maeneo tofauti ndani ya nje ya Tanzania, mshtakiwa Allen kupitia mfumo wa kompyuta unaojulikana kama Mange Kimambi APP, unaosimamiwa na Uturn Collection, alichapisha video ya aliyekuwa Profesa Jay ambaye amelazwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kitengo cha wagonjwa mahututi (ICU) kwa nia ya kusababisha hofu.

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi katika shauri hilo umekamilika na mshtakiwa Mhina anatarajiwa kusomewa maelezo ya awali Aprili 27, mwaka huu.

# Rais Samia aziweka mtegoni TCD, kikosi kazi

Na Paul Mabeja, DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amekiweka mtegoni kikosi kazi cha kukusanya maoni ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa na ile ya uchaguzi.

Amesema ili serikali iliridhie kufanya marekebisho ya sheria hizo, kikosi kazi na TCD vinatakiwa kupeleka mapendekezo ambayo yasiyo na maswali na yamekubalika na wadau wa demokrasia nchini.

Rais Samia alibainisha hayo jana jijini hapo alipokuwa akifungua mkutano wa kitaifa wa haki, amani na maridhiano ulioandaliwa na TCD.

"Mategemeo yetu kikosi kazi kipo kitakuja na yale mtakayojadili na matumaini yangu mtatuletea yale yanayotekelezeka. Mkitupa mazito hatutayatekeleza na itabidi mnune na wanasema 'gabage in, gabage out' (ukiweka taka zitatoka taka). Kwa hiyo mkitutilia 'gabage' hapo zitatoka hivyo hivyo lakini mkiweka mazuri basi tutatekeleza vizuri.

"Sheria ya Vyama vya Siasa inategemeana na mtakavyotuletea. Hili halina shida kama litakuwa halina mkanganyiko lakini kama mtaleta kitu ambacho tunaona kina mkanganyiko basi hakitafanyika," alisisitiza Samia.

Kuhusu ombi la Mwenyekiti wa TCD, Zitto Kabwe, la serikali kutoa ruzuku kwa TCD katika bajeti ya mwaka huu badala ya kuendelea kutegemea wahisani kutoka nje ya nchi, alisema ombi hilo limechelewa.

"Kuhusu serikali kutoa ruzuku kwa kituo hicho katika bajeti ya mwaka huu, umechelewa lakini linazungumzika jambo hili," alisema.

Rais Samia pia aliitaka TCD kujadili na kutoa kwa serikali mapendekezo yanayotekelezeka kwa kuzingatia hali halisi na mazingira ya Tanzania katika majadiliano yao.

"Nawaomba tuzungumzeni kwa mazingira yetu, hali yetu ya siasa, hali yetu ya uchumi na mazingira yetu ya kitanzania. Kama mimi nimetoa roho Rahim kwenu nanyi rudisheni roho Rahim," alisema.

Pia alisema fursa ya kukutana kwa wadau wa vyama vya siasa ni adhimu kwa ajili ya ya kujadiliana na kufikia mwafaka wa kitaifa kama Watanzania.

"Niwaombe tutakayoyazungumza hapa tutazungumza kama Watanzania na sisi ndiyo tutakaoijenga Tanzania yetu. Hakuna mwingine wa kutujengea, watu watatukutanisha na kutulipa posho lakini sisi ndio watu wa kwanza wa kuujenga mshikamano wetu.

"Tunapozungumza maridhiano tunazungumza vipi, tunazungumza yapi, tutakwenda mpaka wapi. Tunaingia kwenye haki zetu kama Watanzania ni zipi kama vyama vya siasa ni zipi na pale tulipofunga haki tuzungumze tutakavyozifungua na tukitoka hapo sasa tunakwenda kudumisha amani ya nchi yetu," alisisitiza.

Mwenyekiti wa TCD, Zitto, alisema mkutano huo ni sehemu ya utamaduni wa kituo hicho kwa zaidi ya miaka 10 sasa.

"Utamaduni huu ni wa zaidi ya miaka 10. Huwa tunafanya mkutano kwa ajili ya kuponya majeraha ambayo vyama vya siasa vimeyapata katika uchaguzi mkuu," alisema.

Pia alisema maazimio ya mkutano huo yatapelekwa kwa kikosi kasi ambacho kitayapeleka kwa Rais.

"Moja ya jukumu la mkutano wa leo ni wajumbe wa kikosi kazi ulichokiunda kusikiliza maoni ya wadau wengine ili kuweza kuboresha maoni yao kabla ya kuyafikisha kwako," alisema Zitto.

Alisema miongoni mwa mambo ambayo wadau wa siasa wamekuwa wakiyalalamikia ni pamoja na sheria ya vyama vya siasa na ile ya uchaguzi.

"Wakati Julai, mwaka huu, nchi yetu inatimiza miaka 30 toka kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi, Mheshimiwa Rais tunaomba sheria hizi zifanyiwe marekebisho katika kipindi hiki cha miaka 30," alisema.


Bank of India (Tanzania) Ltd.

Relationship beyond banking

DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019

MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| NO. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE USD | CHARGE/FEE TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Current Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 500 | 500,000 |
| b) | **Monthly service fee (breakdown per customer)** | | |
| | Folio Charge | 4 | 6,000 |
| c) | Cheque withdrawal over the counter | | |
| | **Up to** Tshs 25,000,000 a day | - | free |
| | **Over** Tshs 25,000,000 a day | - | 0.15% of withdrawn amount |
| | **Up to 5000 USD a day** | free | - |
| | **Over 5000 USD withdrawal** | 0.6% of withdrawn amount | - |
| d) | Fees per ATM withdrawal | - | - |
| e) | ATM mini statement | - | - |
| f) | Interim/additional statement per page | 1.50 | 1500 |
| g) | Periodic scheduled statement | free | free |
| h) | Cheque book **(50 leaves)** | 27 | 42,000 |
| i) | Dishonoured Cheque | 55 | 70,000 |
| j) | Special clearance | | |
| | Within walking distance 1km | 45 | 70,000 |
| | More than 1km | 65 | 95,000 |
| k) | Counter cheque | - | - |
| l) | Inward/Outward cheque collection-USD | 0.60% Min comm. 18 postages USD 90 | - |
| m) | Cancelation of bankers cheque/DD | 15 | 20,000 |
| n) | | | |
| o) | Stop payment | 28 | 35,000 |
| p) | Standing order | - | - |
| q) | Balance enquiry | free | Free |
| r) | Issue of Balance certificate | 7 | 9,000 |
| s) | New ATM card issuance | - | - |
| t) | ATM card renewal or replacement | - | - |
| u) | Overdrawn account interest charge | - | - |
| | - Overdrawn in current account | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| | - Overdrawn in loan account | 2% over regular rate | 2% over regular rate |
| | - Unarranged overdraft | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| v) | Interbank transfer | - | - |
| w) | Bill payments through ATM | - | - |
| x) | **Deposit fee** | - | - |
| | **Savings Accounts** | | - |
| | (Up to USD 5000) | Free | - |
| | (Over USD 5000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| | **Current account.** | | |
| | (Up to USD 10000) | Free | - |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |

| No | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE USD | CHARGE/FEE TSHS |
|---|---|---|---|
| 2.0 | **Savings Accounts** | | |
| a) | Saving bank customer ID Card-one time | 7 | 10,000 |
| b) | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 2,000 | 25,000,000 |
| c) | Cash withdrawal charges over USD 2,000 to 5,000 per day | 0.25% of withdrawal amount | |
| d) | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.60% of withdrawal amount | |
| e) | Cash withdrawal charges over TZS 25,000,000 per day | | 0.10% of withdrawal amount |
| f) | Required minimum opening balance | | |
| | Without Cheque book | 50 | 50,000 |
| | With Cheque book | 200 | 200,000 |
| g) | Monthly service fee | - | - |
| h) | Interim statement | 1.5 per page | 1500per page |
| i) | Cheque book charges 25 leaves | 15 | 20,000 |
| j) | Account closure | 25 | 35,000 |
| k) | **Maintenance of minimum account balance** | | |
| | Without cheque book | 50 | 50,000 |
| | With cheque book | 200 | 200,000 |
| l) | **Minimum balance charges (in case of non maintenance of minimum balance )** | | |
| | Without cheque book | 4 p.m | 900 p.m |
| | With cheque book | 15 p.m | 3,600 p.m |
| 3.0 | **Current Accounts** | | |
| | Ledger folio charges per folio (40lines per folio) | 4 per folio | 6,000 per folio |
| | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 5,000 | 25,000,000 |
| | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.6% of withdrawal amount | - |
| | Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | | 0.15% of withdrawal amount |
| | Cheque book charges 50 leaves | 27 | 42000 |
| | Account closure charges | 70 | 85,000 |
| | **Maintenance of minimum account balance** | 500 | 500,000 |
| | **Minimum balance charges** | 15 p.m | 20,000 p.m |
| 4.0 | **Electronic Banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | - | - |
| b) | Internet transfers | - | - |
| c) | SMS banking | - | - |

| | | Minimum SMS Alert Charge ( to be recovered quarterly upfront) | Number of Free SMS on paying SMS Alert charge | SMS Alert charge per SMS beyond the free SMS (To be recovered in monthly basis) |
|---|---|---|---|---|
| d) | SMS Alert facility - | | | |
| | - **Individual** | free | free | Free |
| | - **Corporate** | free | free | Free |

| No | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| e) | Others | - | - |
| 5.0 | **Foreign Exchange Transaction.** | - | - |
| a) | Purchase/sale of TCs transactions over the counter | - | - |
| b) | Purchase of foreign Cheque. | - | - |
| c) | Sale/purchase of cash passport. | - | - |
| d) | Telegraphic transfer. | | |
| | Remittances Outward(TISS) | 10 | 10,000 |
| | Other Outward remittances: | | |
| | | A/C holder / Non A/C holder | |
| | Up to USD 6,000 | 15 / 40 | -- |
| | USD 6001-10,000 | 30 | -- |
| | Above USD 10,000 | 0.35%max USD 210 | -- |
| e) | Telex/SWIFT. | 30 | - |
| f) | Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank). | | |
| 6.0 | **Other Charges** | | |
| a) | Activation of Dormant Accounts - Per Activation | | |
| | - **Individuals** | 3 | 5,000 |
| | - **Corporate** | 6 | 12,000 |
| 7.0 | **Personal Loans. Charges** | | |
| a) | Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| i) | Personal loans | 1.50% | 1.50% |
| ii) | Overdrafts | 1.50% | 1.50% |
| iii) | Mortgage finance | 1.50% | 1.50% |
| iv) | Asset finance | 1.50% | 1.50% |
| b) | Unpaid loan instalment | 5.00% Over the applicable rate | |
| c) | Early repayment | 2.5% of prepaid loan amount | |
| d) | Valuation fees | As per actual charges by valuer | |
| e) | **Others** | | |
| i) | Documentation charges | Actuals as per advocate bill | |
| ii) | Document Handling Charges | 0.30% of loan amount | |
| iii) | Inspection Charges | Tshs 30,000 per visit | |
| iv) | Modification charges | 0.25% on the sanctioned limit | |
| 8.0 | **Guarantee (Performance/Financial)** | | |
| | Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part there of minimum for one quarter | |
| | Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| 9.0 | **Imports** | | |
| | LC opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| | LC amendment charges | Per amendment 0.40% of LC mount (minimum USD 60 and maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (same for LC against 100% cash margin) | |
| | Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 180 | |
| | Retirement of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Inward Bills for collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| 10.0 | **Exports** | | |
| | Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC advising charges | USD 150 | |
| | Export Bills for collection | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 04.04. 2022 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 04.04. 2022 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 04.04. 2022 |

OTHER DISCLOSURES (VIAMBATANISHI NYINGINEZO)

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.00% p.a. | 14.00% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 3.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 4.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.00% | 5.75% |
| | Over 6 months | 2.50% | 6.75% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.00% | 7.25% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| No. | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 04.04. 2022 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 04.04. 2022 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 04.04. 2022 |

HABARI KITAIFA

# Wafugaji Ngorongoro wataja matakwa kuhamia Handeni

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

WAKATI uandikishaji wa kaya zilizo tayari kuhama katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ukiendelea, wananchi wa jamii ya kifugaji ya Kimasai, wametaja matakwa muhimu wanayotaka yatekelezwe haraka na serikali, baada ya kuamua kuwahamishia Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni mkoani Tanga.

Matakwa hayo ni kuwapo shule ya msingi, zahanati, maji, umeme, barabara na kufanyika haraka maandalizi ya umilikishaji wa hatimiliki za ardhi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wakazi wa Ngorongoro, akiwamo Ngeresai Mathayo, mkazi wa Kata ya Misigyo, alisema ingawa yeye hajajiandikisha bado, lakini kama anakopelekwa kuna shule, zahanati na maji, yuko tayari kuishawishi familia yake kuondoka.

"Serikali ikituambia huko ninakokwenda kuna dispensary (zahanati), shule ya msingi na sekondari, ambayo watoto wangu watasoma, hakuna tatizo, naenda Handeni.

"Nataka niwe na mahali pa kuishi, nataka niwe na shamba la kulima na mahali mifugo yangu itaishi, kwa sababu nategemea mifugo. Huu udongo au ardhi, ndiyo mafuta yetu na tegemeo la uchumi wetu wafugaji."

Aidha, William Leina, Mkazi wa Kitongoji cha Ngereiyani, Kijiji cha Osinoni, Kata ya Kakesio alisema, "Tunaiomba serikali kuweka bayana mambo ambayo yamekuwa yakipigiwa kelele, wakati wa utekelezaji wa zoezi hili.

"Kuna kitu tunataka kujua kama maji, afya na elimu katika eneo hilo la Msomera vipo? Serikali isikae kimya, itoe taarifa kila mara kuhusu hatua iliyofikia katika utekelezaji wa miradi ya huduma za jamii," alieleza Leina.

Pia, Damiani Huho, Mkazi wa Kimba, Kijiji cha Kayapus, Kata Ngorongoro, aliomba serikali ifanye haraka kukamilisha taratibu za uwekaji wa huduma muhimu za jamii ili walio tayari kuondoka kwa hiari, wakaanze kufanya shughuli za uchumi kwa uhuru na upana zaidi, badala ya kuwaacha wenye utayari kushawishiwa na wasiotaka kuhama.

"Nina washawishi watu wa Ngorongoro, ambao hawana hiyo hamasa ya kutaka kuondoka au wanashawishiwa na baadhi ya watu, watumie hii fursa vizuri, maana yake hii fursa haitajirudia.

"Baadaye wakishindwa kuitumia vizuri wenyewe watajuta. Kwa hiyo ni heri watumie fursa hii wafanye maamuzi yao kwa hiari yao ili waweze kubadilisha maisha na uchumi wao kutokana na nchi inavyokwenda."

Vilevile, Paulo Olemurua, mkazi wa Kijiji cha Esere, Kata ya Alaitole alisema: "Tunakuomba Rais Samia Suluhu Hassan, utupeleke mahali pazuri. Maendeleo ni vitu vinne, elimu, maji, barabara na umeme; na sehemu tutakayoishi iwe na usalama. Shule ipo na serikali iko inatulinda sisi. Wekeni ulinzi wa kulinda sisi, hospitali na shule watoto wetu wanaenda kusoma huko.

"Naomba ututoe Ngorongoro mapema kabla kiangazi hakijaingia, kwa sababu mifugo haitaki kuitoa hapa kupeleka kule hatujui tupite nayo wapi tusigombane na wakulima maana sisi ni wageni. Nafuu kuwahi kuondoka, wakati huu wa masika."

Hadi kufikia juzi, mamia ya wananchi waliojiandikisha kukubali kuondoka ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, wanatoka katika Kata za Enduleni, Kakesio, Aleilai, Alaitole, Nainokanoka, Olbalbal, Misigyo, Engaresero, Olorieni na Kata ya Ngorongoro.

Naye, Sara Koromo, Mkazi wa Kata ya Engaresero, alisema kwakuwa wananchi wapo tayari kuhama na kwenda walipotafutiwa na serikali, wanaomba eneo hilo liwe na zahanati ili waondokane na adha ya kutembea umbali mrefu kufuta huduma afya.

Machi 10, mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, baada ya kumaliza kikao chake na viongozi wa mila wa jamii ya Kimasai eneo la Oretei Loongaiki-Marya, kwenye Chuo cha Ufundi Arusha,

Alisema amepokea orodha ya majina ya awali ya kaya 86 zenye watu 453 ambao wamekubali kuondoka kwenye Hifadhi ya Ngorongoro kwa hiari, huku wengine wakiendelea kujiandikisha.

Mafanikio hayo yalitokana na mazungumzo ya Waziri Mkuu aliyoyafanya na wadau wa uhifadhi kwenye vikao vilivyofanyika Februari 14 na 17, mwaka huu katika Tarafa za Loliondo na Ngorongoro.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza wakati wa uzinduzi wa ripoti ya kupinga ukatili iliyoandaliwa na Benki ya Dunia, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mganga mkuu ahamasisha chanjo UVIKO- 19

**Na Sabato Kasika**

KASI ndogo ya chanjo ya ugonjwa wa UVIKO-19 imemshtua

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, na kuwahimiza wakazi wa mkoa huo kujitokeza kwa wingi kupata chanjo ya UVIKO- 19.

Dk. Mfaume alitoa msisitizo huo jana baada ya kubaini kuwa kasi ya watu kupata huduma hiyo bado ni ndogo licha ya serikali kupitia ngazi mbalimbali kuwataka wananchi kujitokeza kuchanja.

Alisema tangu chanjo ilipozinduliwa mwishoni mwa Julai, mwaka jana, hadi kufikia wiki iliyopoita, ni watu 5,71,712 tu ndio ambao wamejitokeza kupata chanjo hiyo katika mkoa.

Katika kikao chake na wenyeviti wa serikali za mitaa kwa lengo la kutaka wahamasishe wananchi kujitokeza kwa wingi kupata huduma hiyo, alisema ni muhimu kwa ajili ya usalama wa afya zao.

Mganga Mkuu huyo alisema wenyeviti wa serikali za mitaa wana mchango mkubwa katika kuhamasisha chanjo na kwamba kila mmoja katika eneo lake afanye hamasa ili wananchi wajitokeze kwa wingi.

"Sasa hivi ninavyozungumza mheshimiwa mgeni rasmi ni tumeachanja watu 5,71,712. Kama una simu unaweza kufanya hesabu hii gawanya kwa 3,800,000 bado tuko chini sana. Hatujafikia hata asilimia 20 ya lengo," alisema Dk. Mfaume.

Dk. Mfaume alisema mkoa umejizatiti katika kupambana kwa kuenea na maambukizi ya UVIKO-19 kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya na serikali kwa ujumla.

Alisema njia nyingine ya kupambana na ugonjwa huo ni kushirikisha viongozi wa serikali za mitaa kwa kuwapa majukumu ya kuhamasisha jamii kwenye maeneo yao ilijitokeze kuchanja.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, N'gwilabuzu Ludigija, ambaye alikuwa mgeni rasmi akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam katika kikao hicho, alisema serikali imeleta chanjo za kutosha ili kila mwananchi achanjwe.

"Mtu akiugua, shughuli za uzalishaji zinasimama na hata uchumi unayumba ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan amejitahidi kuhakikisha analeta chanjo za kutosha, hivyo watu wajitokeze kuchanja," alisema Ludigija.

# WB yapongeza Tanzania kuhusu usawa kijinsia

**Na Salome Kitomari**

RIPOTI ya tathmini ya usawa na ukatili wa kijinsia Tanzania iliyotolewa na Benki ya Dunia (WB) jana, imeonyesha kuwa wasichana maskini wa vijijini wako kwenye hatari ya kutoendelea na elimu ya sekondari ikilinganishwa na wavulana.

Pia usawa wa kiuchumi kati ya wanawake na wanaume umeendelea kuwapo, jambo linalohitaji jitihada zaidi.

Akiwasilisha ripoti ya tathmini ya Jinsia, Kiongozi wa Sekta na Maendeleo Endelevu wa WB, Yaa Oppong, alisema uwiano wa wasichana na wavulana waliondelea na sekondari 78, hali inayoonyesha mafanikio makubwa yapo kwa elimu ya msingi na awali ambako kuna uwiano mzuri.

Alisema kwenye fursa za kiuchumi inaonyesha asilimia 26 ya wanaume wana umiliki wa mali kama nyumba ikilinganishwa na wanawake ni asilimia saba.

Vile vile, tofauti ya umiliki wa ardhi kwa wanawake na wanaume unakadiriwa kuwa kati ya asilimia 20 hadi 30.

Oppong alisema kwa Tanzania Bara asilimia 29 ya wanawake wana akaunti benki ikilinganishwa na wanaume asilimia 44, huku 66 ya wanawake hawamiliki ardhi ikilinganishwa na wanaume (62%) na 51 ya wanawake wanamiliki simu ikilinganishwa na wanaume (69%).

Kwa upande wa Zanzibar, asilimia sita ya wanawake wanamiliki nyumba ikilinganishwa na wanaume (31%), huku wanawake (92%) hawamiliki ardhi ikilinganishwa na wanaume (85%) wanaomiliki.

Alisema, asilimia 16 wana akaunti za benki ikilinganishwa na wanaume asilimia 30, huku (65%) ya wanawake wanamiliki simu ikilinganishwa na 83 ya wanaume.

Alisema vichochezi vya utofauti na ukatili huo ni kiwango kidogo cha elimu, ndoa na mimba za utotoni, kujitegemea kiuchumi, elimu baina ya wanawake, mila, tamaduni na desturi zinazotoa kipaumbele cha elimu kwa mtoto wa kiume, ushiriki mdogo wa wanawake kwenye ajira, tofauti kubwa ya umri kwa wanawake na wanaume na ndoa za wake wengi.

Kiuchumi vichocheo ni malipo duni kwa wanawake, wanaume wengi kumiliki biashara kuliko wanawake, wanawake kukosa umiliki wa ardhi kutokana na mila, kipato duni kinachowafanya washindwe kuwa na akiba na kukosa shughuli za kiuchumi.

Awali, Mkurugenzi Mkazi wa WB nchini, Mara Warwick, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kusema wazi kuwa uwezeshaji wa wanawake utakuwa kipaumbele kwenye utawala wake.

Alisema ripoti hiyo imeonyesha kuwa asilimia 40 ya wanawake wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 49 wamepitia ukatili wa kimwili, huku asilimia 17 wamekutana na udhalilishaji kingono.

Alisema wastani wa wanawake watatu hadi 10 mmoja amepitia ukatili wa kingono na kimwili kabla ya miaka 18 na 44 kutoka kwa watu wa karibu, ikiwa ni kiwango cha juu ikilinganishwa na cha dunia kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mkurugenzi huyo alisema ukeketaji bado ni tatizo kwa asilimia 10 na kwamba mikoa ya Manyara umefikia asilimia 58, huku ukatili dhidi ya watoto ukiwa ni jambo kubwa na asilimia 75 ya watoto wanatendewa ukatili wa kimwili na ndugu kabla ya miaka 18 huku wanawake wa miaka 13 hadi 17 wakipitia hali hiyo miaka mingi iliyopita.

Alisema WB inaishauri serikali kuondoa adhabu ya viboko shuleni kwa kuwa inachangia kwenye ukatili wa kimwili na kingono kwa watoto.

TANGAZO

# MINIMUM DISCLOSURE OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

NMB Close to you

| S/N | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| **1** | **SAVINGS ACCOUNTS** | |
| | Required minimum opening balance | Business saving A/C TZS 100,000, USD 100,EUR 100,GBP 100; Bonus A/C TZS 50,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Mtoto A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Chipukizi A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Pamoja A/C TZS 30,000 |
| | Transaction fee | N/A |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | FREE |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 4,000 ; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Withdrawal bulky without notice | OTC: TZS 4,000 OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Savings Card/Passbook | N/A |
| | Passbook/Card Replacement | TZS 11,800 |
| | Closing Account | TZS 9,440 USD 11.8, EUR 11.8 & GBP 11.8 |
| **2** | **CURRENT ACCOUNT** | |
| | Required minimum opening balance | Business, Supply Chain, Trade Business, Agribusiness Overdraft, Agribusiness Loans, Agri-General, Corporate, Emerging Corporate A/C - TZS 100,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Personal A/C - TZS 15,000; Mwanachuo & Chapchap A/C - TZS 10,000; Wisdom - FREE; Group A/C - TZS 30,000; Fanikiwa A/C - TZS 20,000; Exclusive A/C - TZS 1Million; Executive A/C - TZS 500,000; Kilimo & Bonus A/C - TZS 50,000; Float & Scheme Financing A/C - FREE; Notice Investment A/C - TZS 500Million;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- ZERO |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | Personal A/C - TZS 1,800; Business A/C & Agribusiness - TZS 15,340; Corporate, Insitution & Trade Business A/C - TZS 19,200; Exclusive A/C - TZS 35,400; Executive A/C - TZS 23,600; Emerging Corporate - TZS 19,200; Fanikiwa - TZS 2,000; Personal A/C Agribusiness - TZS 2,048; Kilimo is - TZS 1,800; for Forex A/C charges are Equivalent to TZS;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- FREE |
| | Transaction fee | N/A |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Bank Drafts | NA |
| | Bank Drafts cancellation charge | NA |
| | Cheque book (100 leaves) | TZS 48,380 USD 35.4, EUR 23.6 & GBP 17.7 |
| | Cash Withdrawal at Counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Special Clearance | TZS 53,100 USD 52.8, EUR 46 & GBP 39.5 |
| | Cheque withdraw over the counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Dishonoured cheque | 1.5% of the amount Min 64,000 Max TZS 118,000 |
| | Cash Payment to 3rd party | N/A |
| | Cash Deposit Charge | N/A |
| | Overdrawn account interest charge | N/A |
| | Unarranged Overdraft | N/A |
| | Bulk cash Deposit | FREE |
| | Bulk cash Withdrawal | N/A |
| | Stop Payment orders | TZS 35,400, USD 23.6, EUR 17.7 & GBP 17.7 |
| | Standing Orders ( within the same bank) | FREE |
| | Standing Orders ( to other bank) | TZS 19,710 |
| | Letter of introduction | N/A |
| | Salary handling | TZS 3,540 |
| | School fees deposits | FREE |
| | TRA collection | FREE |
| | Safe custody charges | N/A |
| | Safe custody access fees | N/A |
| **3** | **EFT** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | FREE |
| | To other Banks ( On Others) | 2000 |
| (b) | Outward Transfers | 2000 |
| | Inward Transfers | FREE |
| **4** | **TISS** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | N/A |
| | To other Banks ( On Others) | TZS 10,000 |
| (b) | Outward Transfers | TZS 10,000 |
| | Inward Transfers | FREE |

| 5 | FOREIGN EXCHANGE ACCOUNT | Savings Acc | Current Acc |
|---|---|---|---|
| | Transaction fee | N/A | N/A |
| | Statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | |
| | Interim statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | USD1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month |
| | Withdrawal Charges | 0.25% of the amount - forex | 0.25% of the amount - forex |
| | Cash Deposit Charge | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) |
| | Purchase/Sale of TC transactions over the counter | N/A | N/A |
| | Purchase of Foreign Cheque | N/A | N/A |
| | Sale/ Purchase of cash passport | N/A | N/A |
| | Telex/SWIFT | USD 58 | USD 58 |
| | Transfer from foreign currency denominated account to local account | N/A | N/A |
| | Outward foreign transfers | USD 58 | USD 58 |
| | Inward foreign transfers - Customers | FREE | FREE |
| **6** | **ATM CARD AND TRANSACTIONS RELATED** | | |
| (a) | Local Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | N/A |
| (b) | International Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | Tanzanite - TZS 5,900 ; Titanium - FREE; World Reward - FREE |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800 ; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800 ; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| (c) | ATM Withdrawals: | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | From TZS 1,100 - 1,500 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | TZS 3,540 |
| | ATM mini statement | N/A | TZS 413 |
| | Bill payments through ATM | N/A | FREE |
| (d) | POS | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | TZS 1,770 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | FREE |
| **7** | **MOBILE (SMS) BANKING** | | |
| | Balance Inquiry | N/A | TZS 400 |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers (within NMB) | N/A | TZS 50 - 1300 |
| **8** | **INTERNET BANKING** | | |
| (a) | Domestic: | | |
| | Balance Inquiry | FREE | FREE |
| | Payments | TZS 640 | TZS 640 |
| (b) | International | | |
| | Balance Inquiry | N/A | FREE |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers | N/A | USD 45 |
| **9** | **MONEY REMITTANCES** | | |
| (a) | Western Union | | |
| | Sending | N/A | N/A |
| | Received | N/A | N/A |
| (b) | Money Gram | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (c) | Coinstar | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (d) | Travelex | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (e) | Africash | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (f) | Others (Specify) | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |

| 10 | BANKING SECTOR - DEPOSITS & LENDING RATES | | |
|---|---|---|---|
| A | TYPES OF LENDING RATES | LENDING RATES - PA (%) | |
| | | TZS | USD |
| (a) | Flat | | |
| (b) | Declining | 15% | 9% |
| (c) | Negotiable | | |

**B — FIXED DEPOSITS**

| PERIOD | TZS | | | USD | GBP |
|---|---|---|---|---|---|
| | 500K><9.9Mil | 10M><99.9M | 100M><199M | 2000-49,999 | 2000-49,999 |
| I Month | 2.00% | 2.25% | 2.50% | 0.45% | 0.25% |
| 2 Months | 2.50% | 2.75% | 3.00% | 0.55% | 0.30% |
| 3 Months | 3.00% | 3.25% | 3.50% | 0.70% | 0.40% |
| 6 Months | 3.50% | 4.00% | 4.50% | 0.80% | 0.50% |
| 9 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 12 Months | 5.00% | 6.00% | 7.00% | 1.00% | 0.60% |
| 13-24 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 25-36 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |

**Saving account rates up to 12%**

**Signed By:**

**Aloyse Maro**
**Head Retail Products & Channels**

**Filbert Mponzi**
**Chief Retail Banking**




www.nmbbank.co.tz

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mikakati ya kilimo itekelezwe na ufuatiliaji

**JUZI** Rais Samia Suluhu Hassan, alizindua mpango wa kugawa vitendea kazi kwa maofisa ugani nchini, ambao unalengo la kuboresha kilimo chini ya kaulimbiu ya kilimo na biashara, lengo ni kuwapa hamasa wakulima kuondoa zana ya unyonge, kwa kuwa zipo fursa nyingi za kuondokana na umaskini kupitia kilimo.

Katika hafla hiyo Rais Samia aligawa pikipiki 6,700 zitakazotumiwa na maofisa hao baada ya zingine 300 kutangulia, huku akisema Tanzania inakwenda kufanya kilimo cha kisasa kitakachomkomboa mkulima na kwamba imani yake ni kuwa sekta hiyo inaweza kuikomboa nchi na kuongeza mapato.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema mkakati uliopo ni kupeleka utafiti kwa wakulima badala ya kubaki kwenye makabati.

Alieleza mkakati wa kukabili upungufu wa sukari kwa kuongeza nguvu katika uzalishaji kwenye mashamba ya miwa na viwanda vilivyoingia ubia na sekta binafsi ili kuhakikisha hadi 2025 kusiwe na upungufu. Kwa mujibu wa Msemaji Mkuu wa Serikali, Tanzania inazalisha tani 367,000 za sukari huku mahitaji ni 420,000.

Kwenye mafuta ya kula, Bashe alisema mkakati ulishaanza tangu msimu uliopita kwa wizara kuingilia kati bei ya mbegu za alizeti na kuziuza kwa Sh. 3,500 kilo moja badala ya bei ya wafanyabiashara ambayo ilikuwa Sh. 35,000 kwa kilo.

Hizi ni habari njema hasa ya kugawa vitendea kazi kwa maofisa ugani ambao wanahudumia wakulima wa chini kabisa yaani vijijini ambako ndiko kilimo kipo, tunaamini kwa kuwaahidi umiliki wa vifaa hivyo baada ya miaka miwili kutaongeza morali ya kazi na kuvitunza tofauti na awali ilionekana ni mali ya serikali.

Tunatambua jitihada za sasa za kuinua kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa Tanzania, huku watu zaidi ya asilimia 70 wakiwa vijijini wakikitegemea, pia walioko mjini wanategemea chakula kutoka kwa wakulima, ambao kimsingi mipango ya juu haikuwafikia ipasavyo.

Tuna Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), ambacho tangu kuanzishwa kwake mwaka 1984, na vyuo vingine vya elimu ya kati na vituo vya utafiti wa kilimo, vimekuwa vikitoa wataalamu wa kilimo, vimefanya utafiti wa kuboresha kilimo, lakini bado kilio cha nchi kujitosheleza kwa chakula au kilimo kumkomboa mkulima kiko pale pale.

Tunatambua mabadiliko mengi ikiwamo ya utashi wa kisiasa na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababishwa na uharibifu wa mazingira duniani, kwa kukosekana, kuchelewa au kubadilika kwa vipindi vya mvua, lakini kuondolewa kwa tabaka la juu la ardhi kutokana na kilimo kisicho cha kitaalamu.

Mara nyingi zimezinduliwa programu na mikakati ya kuboresha kilimo zimebuniwa kama tulivyokuwa na kilimo kwanza kwa kutoa matrekta na power tiller kwa wakulima, lakini kutoa mikopo ambayo bado haikusaidia kuboresha na kufikia lengo tarajiwa.

Tunachoona bado elimu waliyopata wasomi wetu hawajajishusha na kuifanya nyepesi ya kueleweka kwa wananchi wa kawaida ambao ndiyo wanafanya kilimo, ilipaswa kuwafundisha kilimo cha wakati wa mabadiliko ya tabia nchi, badala ya kuendelea kuwa na machapisho na kufundisha wataalamu ambao wanashindwa kuhamisha elimu waliyoipata kwenye vitendo.


Zamani tuliona mabwana na mabibi shamba walivyotembelea wakulima kuwapa utaalamu wa kisasa tena hawakuwa na vitendea kazi, sasa tuna teknolojia ambayo unaweza kuzungumza na mkulima kwa simu au kumtumia ujumbe au kutumia vipeperushi na ukamfikia kirahisi bado kilimo kimeshindwa kuwa na tija tarajiwa.

Kama alivyoahidi waziri kuwa watahakikisha utafiti unafika kwa wananchi wa chini kabisa, tunapenda kuona tathmini na ufuatiliaji wa kina unafanyika kila baada ya miezi mitatu au kabla na baada ya msimu wa kilimo ili tuone mabadiliko.

Mara kadhaa, kila mwaka kunapokuwa na maonyesho ya Nanenane utaona mashamba darasa mazuri yaliyoandaliwa kitaalamu yakionyesha tija ya kilimo kwa mavuno mengi kwenye eneo dogo, lakini bado hatujaona matokeo ya maonyesho hayo kubadili maisha ya mkulima zaidi ya kutumia mabilioni ya fedha kwa watendakazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hebu tulinganishe nyayo alikopita Baba wa Taifa, nasi tunakokatiza

Na Sabato Kasika

**ALIPOKUWA** mtumishi wa serikali ya Tanzania, utendaji wake wa kazi ulisadifu kwa dhati fadhila na tunu msingi za maisha ya utu.

Niseme, Mwalimu Julius Nyerere, alikuwa nguzo muhimu ya kuunganisha Watanzania na kuwa wamoja wenye mshikamano na amani, ambavyo vimewaunganisha kwa lugha moja ya Kiswahili na kuwawezesha kutambuana na kuishi kama ndugu licha ya wingi wa makabila yaliyoko nchini.

Ninaamini, bidii yake katika kuwatumikia Watanzania kwa bidii, weledi na uadilifu mkubwa, vitaendelea kumfanya kuwa Mwalimu muhimu wa siasa safi kwa Watanzania na hata nje ya mipaka ya Tanzania.

Kwa mtazamo wangu, amani, mshikamano wa Watanzania umoja wao na maendeleo, mzizi mkuu wa hayo ni Baba wa Taifa, kwani hilo hakulifanya tu kwa Tanzania, bali hata kwa mataifa mengine.

Ninaamini kuwa wale waliofuatilia historia yake, watakuwa wanamjua wajihi wake, alikuwa yu daima tayari kusaidia mataifa mengine ya Afrika kujikwamua katika madhila ya harakati za ukombozi, umaskini, misukosuko na hali tete ya kisiasa.

Alisisitiza mambo mengi kuanzia masuala ya uchumi, siasa na dini na ukabila, ambalo ni nyeti Baba wa Taifa aligusa katika hotuba nyingi alizowasilisha akiukemea kwa kuwa alijua madhara yake.

Mwalimu Nyerere, amekemea suala la ukabila kila alipopata nafasi ya kuzungumza na hakutaka kuwapo maswali kama 'wewe ni kabila gani', kwa kiasi kikubwa alifanikiwa kwani hadi sasa Watanzania hawaulizani kabila.

Nyerere aliamini katika itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea na hakutaka udini upewe nafasi, kwa kuwa alijua kwamba mambo hayo yakichochewa na kupewa nafasi hayana simile, ikifika wakati ukashika kasi hakuna wa kuzuia.

Kwenye suala la uongozi na maadili ya uongozi, ni jambo ambalo Baba wa Taifa aliliweka mbele, kwa lengo la kupata viongozi ambazo wanawatumikia Watanzania badala ya kufanya kazi kwa manufaa binafsi.

Hata alipoona ndani ya CCM mambo yanakwenda ndivyo sivyo, hakusita kutamka haradharani kuwa Watanzania wanataka mabadiliko, wasipoyapata ndani ya CCM, watayapata nje ya CCM.

Kauli hiyo inaonyesha wazi kuwa alikuwa na dhamira ya dhati ya kutaka viongozi wawe wa serikali au chama, kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ili waaminike kwa wananchi badala ya kwenda kinyume.

Aidha, alitamani kuunganisha nchi za Afrika Mashariki, na kuwa na uongozi wa pamoja, ingawa hakufanikiwa katika hilo, lakini akafanikiwa kuunganisha Tanganyika na Zanzibar na kuwa na nchi moja inayoitwa Tanzania.

Yapo mengi ambayo Baba wa Taifa alikuwa akiyasisitiza katika uongozi wake na hata baada ya kung'atuka, lakini lingine zaidi ni suala la kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini mwaka 1992.

Kabla ya kurejeshwa kwa mfumo huo, iliundwa tume ya kukusanya maoni ya Watanzania ili kuona kama wanautaka mfumo huo, asilimia 80 ya Watanzania walitamani kuona nchi inaendelea kuwa na mfumo wa chama kimoja.

Hata hivyo, Baba wa Taifa aliingilia kati na kushawishi Watanzania kuingia katika mfumo wa vyama vingi kwa kuwa isingekuwa busara kwenda kinyume na mabadiliko ya dunia na pia isingekuwa vyema kuwapuuza asilimia 20 waliotaka mfumo wa vyama vingi.

Baada ya maelezo hayo, ndipo nchi ikaingia ndani ya mfumo huo, huku vyama vya siasa vikianzishwa kama utitiri na kisha uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo huo ukafanyika mwaka 1995, kurejea ilivyokuwa kabla ya mwaka 1964.

Wakati makongamano, shamrashamra na mambo mengine, maeneo mbalimbali kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 100 tangu alipozaliwa Baba wa Taifa, ni muhimu kukumbuka mchango wake kwenye mageuzi nchini.

Ingawa kuwa na mfumo wa vyama ilikuwa ni kwenda kinyume na matakwa ya Watanzania wengi, matamanio yake yalikuwa ni kwamba, Watanzania wanaotaka kushiriki siasa nje ya CCM wasibanwe bali wawe huru.

# DC ashtukia udanganyifu ujazo wa vyakula vya Mwezi Mtukufu

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, ameshtukia udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wa vyakula vya mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani katika masoko ya mji wa Iringa kwa kuwapunja wateja.

Kutokana na hali hiyo, ameagiza maofisa wa vipimo na maofisa biashara kuchunguza na kuwachukulia watu wanaofanya vitendo hivyo.

Moyo alitoa agizo hilo juzi baada ya kutembelea masoko mbalimbali ya mji wa Iringa akiwa ameongozana na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ili kufanya uchunguzi kutokana na malalamiko ya baadhi ya wananchi kuhusu udanganyifu wa wafanyabiashara wa vipimo vya vyakula vinavyotumika katika mfungo wa Mwezi Mtukufu.

Baada ya kubaini tatizo hilo, Moyo alisema udanganyifu huo haukubaliki na kuagiza hatua stahiki zichukuliwe haraka.

Alisisitiza kuwa kitendo cha baadhi ya wafanyabiashara kutumia vipimo visivyo sahihi kuuza vyakula ni kinyume cha sheria na sawa na wizi kama wizi mwingine na kuwa kwa wale watakaobainika kufanya wizi huo, hatua kali zitachukuliwa dhidi yao. "Unapopanga bei ya kilo moja ya bidhaa yoyote ile ni lazima kipimo kinachotumika kiwe kina ujazo wa kilo moja na kipimo sahihi ni mzani pekee unaoweza kuonyesha uhalisia wa ujao husika na si tabia ya baadhi ya wafanyabiashara kuuza bidhaa zao kwa kukadiria ujazo," alisema.

Alisema iwapo tabia hiyo itaachwa hivyo anayeumizwa na mlaji anayenunua bidhaa husika, hivyo si sawa kuona bidhaa mbalimbali zikiendelea kuuzwa kwa vipimo vya kukisia.

Moyo aliwataka maofisa masoko katika masoko yote ya wilaya ya Iringa kwa kushirikiana na maofisa biashara pamoja na watu wa vipimo kupita katika maeneo yote ya biashara kuchunguza aina za vipimo vinavyotumika kupimia bidhaa na wale wanaouza kwa vipimo visivyo halisi wachukuliwe hatua.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara wa tambi katika soko kuu la mjini Iringa, Juma Ally alisema imekuwa vigumu kupima tambi kwenye mzani kwa madau kuwa zitaingia nyingi zaidi na wao wanakujumlishiwa wamekuwa wakiuziwa pasipo kupima kwenye mizani .

Alisema kwa sehemu kubwa bidhaa hiyo wamekuwa wakiuza kwa kukadilia ujazo kwenye vifungashio na si kupima kwenye mizani .

Kutokana na agizo hilo la mkuu wa wilaya, alisema ni wazi kuwa watapata hasara kubwa na kuomba kumalizia mzigo huo kwa kutumia vipimo walivyozoea kabla ya kuanza utekelezaji.

Katika hatua nyingine, Moyo alisema Halmashauri ya Manispaa ya Iringa imeanza kuweka uzio katika eneo la makaburi ya Mlandege kwa lengo la kuwezesha wafanyabiashara wadogo (machinga) kutumia sehemu ya eneo hilo kufanya biashara kama walivyoomba.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (kulia), akikagua bei na vipimo vinavyotumika kuuzia bidhaa za vyakula wakati wa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, alipofanya ziara na kamati ya ulinzi na usalama wilaya hiyo, katika soko kuu la Manispaa ya Iringa, jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Kunenge awashukia madiwani wanawake

**Na Julieth Mkreri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amewataka madiwani wa viti maalum katika mkoa kutambua nafasi zao na kutekeleza majukumu kwa kuleta matokeo chanya hasa katika kutatua kero za wananchi waliowachagua.

Kunenge aliyasema hayo jana mjini hapa alipokuwa akifungua mafunzo kwa madiwani wanawake 54 ambayo yameratibiwa na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Pwani, Hawa Mchafu, kwa ufadhili wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Alisema wajibu wa madiwani hao ni kutambua majukumu waliyo nayo na kufahamu matarajio ya wananchi kwa kutatua vikwazo vya maendeleo vinavyowakabili.

"Ni wajibu wenu kusimamia matarajio ya waliowaamini. Wananchi wanataka kuona matokeo chanya, hivyo fanyeni lililo sahihi katika kutekeleza majukumu yenu ili kazi yenu itambulike mwaka 2025 kwa kuwa na matokeo chanya ya kazi zenu," alisisitiza Kunenge.

Akizungumzia suala la ndoa za utotoni na unyanyasaji wa kijinsia, Kunenge alisema ni lazima kuyaibua mambo hayo kwenye jamii na kuyaundia mikakati ya kuyamaliza.

Mkuu wa Mkoa aliwataka madiwani hao kushirikiana na serikali katika mambo mbalimbali ikiwamo kuwahamasisha vijana kuchangamkia fursa za ajira kwenye viwanda badala ya kuwaachia wale wa kutoka mikoa mingine kufanya kazi katika viwanda vilivyopo.

"Tusipobadilika mkoa wetu utaendelea kubaki kuwa watazamaji. Vijana wetu wanalalamika malipo madogo wakati wako wengine wanatoka mikoa ya jirani wanakuja kunufaika na ajira hizo hizo. Mnatakiwa na nyie madiwani muongee na vijana wetu wabadilike. Hao wanaokataa kazi wanabaki mtaani bila shughuli yoyote," alisema.

Mbunge Hawa Mchafu alisema mkoa bado unakabiliwa na kikwazo cha ndoa za utotoni, mimba na utoro hali iliyosababisha kuandaa andiko kwa LHRC ili madiwani wanawake wapatiwe mafunzo.

Alisema mafunzo hayo pia yalikuwa na lengo la kuwajengea uelewa madiwani kuwa na uwezo wa kujenga hoja kwenye vikao vya madiwani katika miradi ya maendeleo.

"Katika mkoa wetu kero tuliyo nayo ni utoro, mimba za utotoni na mila na desturi ambazo si rafiki kwa mtoto wa kike. Nimeona nichague madiwani hawa wanawake wa kata na viti maalumu wajengewe weledi ili waone tatizo liko wapi," alisema.

Alisema madiwani wengi walikuwa wanarudi nyuma badala ya kutoa ushirikiano na kwamba kikwazo kilikuwa katika eneo la mahakamani, hivyo kuanzia sasa watakuwa na ujasiri wa kufuatilia kesi hizo hadi mwisho.

# Tanzania, Uingereza kushirikiana vita usafirishaji haramu binadamu

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA na Uingereza zimekubaliana kuweka mikakati ya pamoja kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu wakiwamo watoto hasa maeneo ya mipakani.

Hayo yalibainika juzi jijini Dar es Salaam wakati wa ziara ya Waziri wa Uingereza anayeshughulikia Masuala ya Afrika, Vicky Ford, iliyolenga kujadiliana na kutafuta suluhu ya tatizo la usafirishaji haramu wa binadamu wakiwamo watoto.

Akizungumza baada ya ziara hiyo kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alisema Uingereza imeahidi kutoa jengo maalum kwa ajili ya kutoa huduma za pamoja kwa ajili ya kusaidia waathirika wa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Kwa mujibu wa Dk. Chaula, misaada hiyo itakuwa katika huduma za afya, ushauri wa kisaikolojia, msaada wa kisheria na huduma za polisi katika eneo moja ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hizo.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha suala hilo linapatiwa ufumbuzi, uwajibikaji wa pamoja unahitajika kwa wataalamu mbalimbali wanaohusika na kusaidia waathirika wa vitendo vya ukatili ili kusaidia kutoa huduma stahiki kwa uharaka na urahisi kwa kuokoa jamii.

"Huduma hizi zitapatikana hapa hapa katika eneo moja na hasa kwa kushirikiana na serikali ya Uingereza. Tumekusudia kubadili mazingira na kuleta huduma za pamoja kwa wahanga (waathirika) wa vitendo vya ukatili katika jengo la British Council na hii itakuwa kwa kuanzia na maeneo haya yatasambaa kila mkoa," alisema.

Naye Waziri Ford alisema tatizo la usafirishaji haramu wa watu linaongezeka kwa kasi hasa katika mipaka, hivyo kutishia ustawi wa jamii hasa watoto.


Alisema Uingereza iko tayari kushirikiana na Tanzania hasa katika kuweka mikakati ya kuhakikisha tatizo la usafirishaji haramu wa watu hasa watoto linapungua kama si kutokomezwa kabisa.

"Usafirishaji haramu wa watu ni shida. Ni tatizo kubwa hasa kwa nchi za Afrika ambazo zimekuwa njia ya kusafirisha watu kwenda nchi za Ulaya. Tudhibiti hili tuiokoe jamii yetu," alisema.

Naye Meneja wa Simu ya Huduma kwa Mtoto 116, Thelma Dhaje, alisema uwapo wa vituo vya pamoja vya kutoa huduma kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, utasaidia kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma muhimu kwa waathirika na kuwahakikishia upatikanaji wa haki kwa wanaofanyiwa vitendo hivyo.

Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala, Asia Mkene, alisema uwapo wa kituo cha pamoja cha kutoa huduma kwa waathirika wa vitendo vya ukatili, utakuwa suluhisho kwa kuhakikisha huduma zote zinapatikana kwa wakati katika eneo moja na kuharakisha utoaji huduma.

## TANGAZO


mdundo
Mdundo Inakutakia Ramadan Karim Kwa Ajili Yako Na Familia Yako
Tafakari kuhusu Allah kupitia Mix nzuri za Kaswida.
Tembelea www.mdundo.com/djmixes.
MUSIC
GET NEW DJ MIXES EVERYDAY
only on mdundo.com

# Mazingira magumu wapatiwa mil. 16/- kuanzisha miradi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAZAZI na walezi wa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu wanasoma katika kituo kinacholea watoto wenye mahitaji maalumu cha FPCT, wilayani hapa wamepatiwa msaada wa miradi ya ujasiriamali yenye thamani ya Sh. milioni 16 kuwapunguzia umasikini wa kipato.

Hayo yalisemwa jana wilayani hapa na mratibu wa kituo hicho tawi la Masasi, Edmund Mahene, alipokuwa akizungumza na gazeti hili kuwa wanawalea watoto waishio katika mazingira magumu na kuwasaidia mahitaji mbalimbali ya msingi ikiwamo chakula, mavazi, stadi za kazi pamoja na huduma za kiroho.

Alisema kituo hicho kipo chini ya kanisa la Free Pentecostal Church of Tanzania (FPCT) lililopo mjini Masasi, kinaelea watoto wenye uhitaji maalumu huku wazazi pamoja na walezi wa watoto hao hupatiwa miradi ya ujasiriamali ili iweze kuwainua kiuchumi na kuondokana na hali ngumu ya maisha.

Mahene alisema watoto hao ambao baadhi yao ni yatima, wanahudumiwa kupitia maeneo makuu manne la kwanza ni mtoto kuhudumiwa kimwili kwa kupatiwa matibabu bora ya kiafya, eneo la pili ni kuhudumiwa kijamii, kiuchumi na kielimu.

"Lengo la kuwawezesha wazazi na walezi hawa kwa kuwapa miradi hii ya ujasiriamali tunajua wakiwa na kipato wazazi itakuwa rahisi kuwahudumia watoto wao na pale tunapomuwezesha mtoto kiuchumi kwa kumpatia elimu na stadi za kazi pia itakuwa rahisi kwao baadaye kupata kipato na kuwasaidia wazazi wao," alisema Mahene.

Alisema katika eneo la kiuchumi watoto hao wanafundishwa pia elimu ya kujitegemea ambayo itawawezesha kujitegemea kwenye maisha ya baadaye na kuzisaidia familia zao.

Alisema licha ya kubeba jukumu la kulea watoto hao pia kituo hicho kinawawezesha kiuchumi wazazi na walezi wa watoto wanaosoma kwenye kituo hicho na tayari wazazi hao wamepatiwa msaada wa miradi ya kiuchumi ya Sh. milioni 16 hatua ambayo itawawezesha kupata kipato na kuendesha maisha yao.

Mmoja wa mwalimu anayefundisha katika kituo hicho, Joyce Nyambo, alisema amebaini uwapo wa vipaji vikubwa kwa watoto hao ikiwamo cha uchoraji, kuimba na kuigiza na kwamba wakiendelezwa itawasaidia katika maisha yao.

Akizungumza na gazeti hili mmoja wa wazazi ambaye mtoto wake anasoma katika kituo hicho, Asha Dadi alisema anakishukuru kituo hicho kwa kumpatia mradi wa saluni ya kike yenye vifaa vyote vinavyohitajika na kupitia saluni hiyo anaweza kupata kipato na kuendesha maisha yake tofauti na alipokuwa hana.

# Achukizwa usajili anwani za makazi kusuasua

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Hashimu Komba, amewahimiza viongozi wa vijiji, kata na tarafa, kusimamia usajili wa anwani za makazi kwa kuwaelimisha wananchi umuhimu wake.

Komba alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza na viongozi wa wilaya hiyo, wakiwamo madiwani, Nachingwea mjini.

Alionyesha kusikitishwa na kasi ndogo ya utekelezaji wa kazi inavyoenda kwa kusuasua katika baadhi ya kata na maeneo mengine kutoanza kabisa.

Alisema kati ya nyumba 82,000 zinazohitajika kusajiliwa ni 17,000 pekee zilizosajiliwa, wakati 65,000 bado hazijasajiliwa huku akizitaja kata za Nachingwea mjini na Boma kutoonyesha juhudi za utekelezaji wake.

"Mfano Kata ya Boma imesajili nyumba 27 tu, Kata ya Nachingwea mjini ipo ziro kabisa, haijawahi kusajili hata moja," alisema Komba.

Alisema usajili wa anwani ya makazi una umuhimu wake kwa baadhi ya utoaji huduma, kwa kuwa itarahisisha sensa ya watu na makazi inayotarajia kufanyika mwaka huu.

Komba aliwahimiza viongozi wakiwamo madiwani kusimamia kwenye maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuelimisha wananchi umuhimu wake kwa kuwa serikali inahitaji kuingiza kwenye mfumo wake.

"Viongozi wenzangu kutokana na idadi ndogo ya usajili huu, ipo haja ya kwenda kusimamia utekelezaji wake kwenye maeneo yenu," Komba alisisitiza.

Baadhi ya viongozi akiwamo Diwani Kata ya Nachingwea mjini, Mustafa Ngonyani, alisema baada ya kupata taarifa hiyo, wanakwenda kujipanga kuhakikisha usajili wa anwani za makazi unafanikiwa katika maeneo yao ili kuiwezesha serikali kupanga majukumu yake.

"Mimi sikuwa nafahamu kama kwenye kata yangu kuna ziro narudi nyumbani kujipanga na watendaji wangu," alisema Ngonyani.




Mtaalam wa Bidhaa za intaneti wa Tigo, Blass Abdon, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa simu janja mbili za Infinix Smart 6 na Infinix 12i. Kulia ni Ofisa Uhusiano wa Infinix Tanzania, Aisha Karupa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara ya Afya yapokea vifaa vya mil. 203/- toka USAID

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Afya imepokea vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) vyenye thamani ya Sh. milioni 203.5 kutoka Shirika la USAID kwa kushirikiana na JHPIEGO kupitia mradi wake wa Momentum Challenge Global Leadership (MCGL).

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Abel Makubi, akizungumza wakati wa kupokea msaada huo jana mkoani Dar es Salaam, alitaja vifaa hivyo ni kompyuta za mezani 75 ambazo kupitia idara yake ya mafunzo zitasambazwa kwenye vyuo vya kada za afya sita na wizarani.

Prof. Makubi aliishukuru USAID kwa mchango wao mkubwa ambao utaboresha mafunzo ya TEHAMA vyuoni na utasaidia kuzalisha wataalamu wa afya wenye ujuzi na umahiri kwenye matumizi hayo nchini.

Aliongeza kuwa, vifaa hivyo pia vitachangia kuboresha huduma za mafunzo na amevitaka vyuo vyote vitakavyonufaika na vifaa hivyo kuvitunza na kutumia kwa shughuli zilizokusudiwa.

Hata hivyo, Prof. Makubi aliwataka wakuu wa vyuo vya afya nchini kuzingatia weledi na maadili ya utumishi wa umma kwa maendeleo ya taifa.

"Ni wakati muafaka kwenu ninyi viongozi kufanya kazi kwa bidii na kuhakikisha kuwa mnazingatia maadili yote ya kitaaluma ili mzalishe wataalamu wenye uwezo katika kusaidia utoaji wa huduma za afya zenye ubora.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa USAID Dk. Patrick Swai, alisema Shirika hilo litaendelea kuisaidia Wizara ya Afya kuboreaha utoaji wa huduma za afya nchini.

Dk. Swai aliongeza kuwa Tanzania ni nchi mojawapo zilizopewa kipaumbele katika mpango wa kushughulikia vifo vinavyoweza kuzuilika vya wajawazito na watoto.

Naye Mkurugenzi wa Jhpiego nchini, Alice Christensen, alisema Shirika lake litaendelea kuunga mkono jitihada za serikali na kuahidi kuwa mshirika hai katika kuleta mabadiliko sekta ya afya.

# Wizara yaomba kibali ajira askari 600

WIZARA ya Maliasili na Utalii, imeomba kibali cha kuajiri askari 600 wa wanyamapori ili kusaidia kudhibiti wanyama wakali na waharibifu.

Naibu Waziri Mary Masanja aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Minza Mjika.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali wa kudhibiti na kutoa fidia kwa wananchi wa mkoa wa Simiyu wanaopakana na hifadhi za wanyamapori na kuathiriwa na wanyama hao.

Akijibu swali hilo, Masanja alisema katika kukabiliana na tatizo hilo, wizara imeendelea kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kusimamia utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori wa mwaka 2020/21 - 2024/25.

Alisema miongoni mwa mambo yaliyomo kwenye mkakati huo ni kufanya doria za mara kwa mara kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu.

"Aidha, Mheshimiwa Rais alielekeza vijengwe vituo vya askari katika maeneo ya Busega na Meatu. Mchakato wa ujenzi umeanza ambapo vituo viwili vitajengwa katika maeneo tajwa Aprili, mwaka huu. "Sambamba na hilo, maombi ya vibali vya kuajiri askari 600 ameshawasilishwa kwenye mamlaka husika," alisema.


Jambo lingine, alisema ni kutoa mafunzo ya mbinu za kujilinda na kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu na halmashauri za wilaya 17 zimepatiwa mafunzo hayo.

Pia alisema wizara ina namba maalum za simu kwenye kila kanda za kiutendaji ili wananchi watoe taarifa za matukio ya wanyamapori bila malipo.

"Mheshimiwa Spika, malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi kwa mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya Sh. milioni 790.72 zimetolewa kwa wananchi 3,598," alisema.

Hata hivyo, alisema wizara imepokea maombi ya malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi kutoka wilaya mbalimbali zikiwamo wilaya za mkoa wa Simiyu.

Alisema kwa sasa wizara inafanya uhakiki wa maombi hayo kabla ya malipo kufanyika.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akimwapisha Mbunge wa kuteuliwa, Shamsi Vuai Nahodha, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Mabehewa 22 ya abiria kuwasili Aprili

BUNGE limeelezwa kuwa mabehewa mapya 22 ya treni ya abiria yanatarajiwa kuingia nchini Septemba, mwaka huu.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), Kilumbe Ng'enda.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali wa kuboresha usafiri wa reli ya Kigoma - Dar es Salaam ambao umezorota kutoka safari moja kila siku kufikia safari mbili kwa wiki.

Akijibu swali hilo, Mwakibete alisema Shirika la Reli Tanzania (TRC) limetia saini mkataba wa ununuzi wa mabehewa hayo mapya abiria 22.

Kwa sasa, alisema TRC inafanya safari mbili kwa wiki kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma na hali hiyo inatokana na uhaba wa mabehewa ya abiria.

"Ili kuondokana na upungufu wa mabehewa, shirika lilianza taratibu za kukarabati mabehewa 37 na Juni, 2021 ulitiwa saini mkataba wa ununuzi wa vipuri kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa hayo," alisema.

Alisema vipuri hivyo vinatarajiwa kuingia nchini mwisho wa Aprili, 2022 na vitakapowasili kazi ya ukarabati itaanza.

"Kazi hiyo ya ukarabati inatarajiwa kufanyikwa kwa miezi minane hadi Desemba, 2022 kupitia mafundi wetu wa ndani," alisema Mwakibete.

Aliwaomba wananchi wa Kigoma kuwa na subira wakati serikali inaendelea na ukarabati na ununuzi wa mabehewa ya abiria.

"Baada ya utekelezaji wa kazi hizo, idadi ya safari za treni kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma zitaongezeka kutoka safari mbili hadi nne kwa wiki," alisema.

Katika swali lake la nyongeza, mbunge huyo alihoji mpango wa kukarabati mabehewa mengi zaidi badala ya kununua mapya ambayo ikianza reli mpya ya kisasa (SGR) yataachwa.

Akijibu swali hilo, Mwakibete alisema mabehewa hayo yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 14.9 yatakwenda Kigoma.

"Bado tutaendelea kukarabati mabehewa tuliyonayo kwa kuwa bado tutaendelea kutumia reli iliyoko ya sasa," alisema.

## Magari 369 ya polisi kuongeza utendaji

SERIKALI imesema inatarajia kupokea magari 369 kutoka nchini India ifikapo Septemba, mwaka huu, kukabiliana na uhaba wa magari kwenye vituo vya polisi.

Magari hayo yatakapofika yatagawiwa kwenye vituo vya polisi vyenye uhitaji mkubwa na mwishoni mwa mwezi huu, serikali itapokea magari 78 yaliyokaguliwa na kuthibitishwa.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zuena Bushiri.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kununua magari mapya ya polisi kwa ajili ya vituo vyake ili kupunguza uhaba wa vitendea kazi hususan magari katika jeshi hilo.

Akijibu swali hilo, Waziri Masauni alisema serikali inatambua umuhimu wa kulipatia Jeshi la Polisi magari kama nyenzo ya kutendea kazi.

Kupitia mkataba kati ya serikali na kampuni ya Ashok Leyland ya India, alisema serikali inatarajia kupokea magari hayo.

Katika swali la nyongeza la mbunge huyo, alisema mkoa wa Kilimanjaro una uhitaji wa magari hayo hasa ya doria.

"Serikali ina mpango gani mkoa wa Kilimanjaro kupata magari katika awamu hii ya kwanza ya magari 78 yanayoingia nchini mwezi Aprili?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Masauni alisema amepokea mapendekezo hayo na kuhakikisha magari yatakapofika Mkoa huo utapewa kipaumbele.

Naye Mbunge wa Temeke (CCM), Dorothy Kilave, alihoji serikali ina mkakati gani wa kutenga bajeti ili kutengeneza magari mabovu yaliyoko kwenye vituo vya polisi wakati yakisubiriwa magari mapya.

Akijibu swali hilo, Masauni alisema kuna kitengo ndani ya Jeshi la Polisi cha kutengeneza magari na serikali inatarajia kuja na mpango wa kutatua tatizo hilo na wakati wa bajeti yetu tutakuwa na nafasi kubwa ya kufafanua,"alisema.




Habari zote na Augusta Njoji



Ukurasa 12

**Karata kuu tatu zinazobaki mtaji CCM, wazee ndio rasilimali kuu**



Ukurasa 13

Makomredi Mangula, Kinana, uzao wao unadumu kwa kuilinda CCM


siasa

JUMATANO APRILI 6, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 14

**Mwafrika wa kwanza kuongoza ILO**

# Misukosuko inayomkabili Raila Odinga kusaka urais mara ya 5

**Na Christina Mwakangale**

HARAKATI za Raila Odinga, kuwania urais nchini Kenya na yale anayopitia kuelekea uchaguzi mkuu wa Agosti mwaka huu, bado kuna wingu kwa anayoyatarajia kupata, sasa mara yake ya tano.

Raila anaungwa mkono na takribani vyama 20 vinavyotambulika kwa jina Azimio la Umoja, bila kumuweka kando Rais Uhuru Kenyatta, ambaye mara kadhaa ameonyesha kile anachokiita haki ya kisiasa ya kumuunga mkono mtu yeyote.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa, wanasema kwamba kiongozi huyo, sasa ni nafasi yake muhimu zaidi kuwania nafasi hiyo.

Kenyatta, amesikika hivi karibuni akitamka: "Najua wapi nataka kura yangu iende na ni haki yangu. Au nimefanya kosa lolote? Ikiwa unataka kura, basi iombe tu! Nikisema namuunga mkono Baba (Raila), haimaanishi kuwa mtu mwingine ni mbaya,"

Anaendelea: "Uamuzi juu ya nani ataongoza, kama vile wajibu wetu ni mapenzi ya Mungu anapozungumza kupitia sisi. Kwanini basi tupigane na kuuana sisi kwa sisi? Tupige kura tuendelee na shughuli zetu huku tukisubiri matokeo kutangazwa."

Kenyatta amebainisha hayo wiki hii, ikiwa ni saa chache tu baada ya Raila kuvamiwa na vijana na kurushiwa mawe, kitendo ambacho Rais amekilaani.

Kenyatta alikuwa akizungumza baada ya kuhudhuria ibada kanisani jijini Nairobi siku ya Jumapili iliyopita, alikofungua rasmi chuo cha mafunzo na kisha akajiunga na waumini kwa ajili ya ibada.

Rais Kenyatta, alikemea siasa zilizo na fujo na ghasia na kuwataka viongozi wa kisiasa wafanye kampeni zao kwa njia ya amani bila ya kutowagombanisha Wakenya.

Mkuu huyo wa nchi ambaye baba yake Mzee Jomo Kenyatta, alikuwa kiongozi wa nchi na mshindani wa baba wa Raila, Mzee Jaramogi Oginga Odinga, anawataka Wakenya kuachana na siasa za ghasia.

Anasema, badala yake waandamane kwa ajili ya amani na umoja wa nchi, akifafanua: Tunataka nchi ambayo hatuonani kama maadui bali ndugu na dada".

Anasema kwamba uchaguzi siku zote huja na kupita kila baada ya miaka mitano, ila nchi itabaki na hakuna atakayeondoka nchini humo baada ya uchaguzi, hivyo ipo haja ya kuilinda.

"Hakuna haja ya vurugu. Mbona unapiga mawe helikopta iliyombeba Baba? Je, hilo litakusaidiaje? Ikiwa athari yeyote ingetokea kutokana na hilo, je, nchi isingeingia kwenye moto? Ndivyo tunataka?" amesisitiza rais, akikemea kitendo hicho.

"Tuombe kura kwa njia ya heshima na amani."

Rais Kenyatta, amesema hawezi kubadili uamuzi wake kuhusu kumuunga mkono mshirika wake, akisema ni haki yake kumuunga mkono yeyote anayeona anafaa kumrithi.



Raila Odinga akiwa katika safari ya kampeni zake. **PICHA: MTANDAO**

### ASHAMBULIWA MAWE

Mwishoni mwa wiki, Raila Odinga, anayewania urais kupitia Azimio la Umoja One Kenya alipigwa mawe na kulaumu shambulio dhidi yake lililotokea akiwa katika helkopta eneo la Kabenes, Kaunti ya Uasin Gishu.

Anasema kundi la vijana lilimvamia wakati akiondoka eneo hilo kuelekea Ortum, Alale na Lomut, kuendelea na kampeni na kudai kwamba mawe yalirushwa akiwa pamoja na ujumbe wake, wakati wakielekea kupanda helkopta.

"Sisi hatujapiga mtu yeyote. Wala hatujafanya fujo pahali popote, tunalaani. Jana mimi nimeona vioja. Vijana wanakuja sisi tulitoka kutoa pole kwa familia alafu wakaanza kupiga magari yetu mawe.

"Mawe yalinyesha kama mvua kwa gari langu. Wakipiga, nikauliza ni nini inafanyika. Vijana wakangoja nikiingia kwa ndege alafu nikaona mtu anarusha mwamba mkubwa na sikuwa na pahali pa kuenda. Nilishangaa, ni mambo gani haya. Jamaa walitaka kuua sisi."

### WANASWA 17

Katika tukio hilo, Jumatatu wiki hii, watuhumiwa 17 wamefikishwa mahakamani mjini Eldoret, wakihusishwa na shambulizi dhidi ya mgombea urais kupitia muungano wa Azimio la Umoja- One Kenya.

Kabla ya tukio hilo, Raila Odinga alikuwa akitokea eneo la Kabenes, Kaunti ya Uasin Gishu, kuhani msiba, mwishoni mwa wiki.

Washukiwa hao wanadaiwa kuhusika na shambulizi la kupiga mawe helikopta aliyokuwa imembeba Raila, ambaye ni kiongozi wa chama cha ODM, eneo la shamba la marehemu Mzee Jackson Kibor la Samitui, muda mfupi baada ya mazishi.

Wanashitakiwa kwa jaribio la mauaji, uchochezi wa ghasia, uharibifu wa mali na uvunjifu wa amani. Wahusika wako mahabusu.

Raila alitembelea shughuli za mazishi na kukumbwa na tukio hilo.

Mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Mashtaka (DCI) amesema uchunguzi wa awali umeanza na kwamba wabunge wawili akiwamo wa Soi, Caleb Kositany na mwenzake wa kaunti ya Uasin Gishu, David Kiplagat, walihojiwa eneo la makao makuu ofisi ya DCI, mjini Nakuru.

Rais Uhuru Kenyatta amelaani tukio hilo akisema linahatarisha amani na usalama wa nchi hiyo na linaweza kuchochea uvunjifu wa amani.

***• Kwa mujibu wa taarifa za mtandao.***

ALICHOPANDIKIZA MWAKA 1954...

# Karata kuu tatu zinazobaki mtaji CCM, wazee ndio rasilimali kuu



Mama Maria Nyerere wa kwanza kushoto, akiwa na Mama Salma Kikwete, Mama Fatuma Karume pamoja na wajumbe wengine wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) katika ukumbi wa Jakaya Kikwete mjini Dodoma kuhudhuria mkutano huo Desemba 8, 2017. **PICHA: MTANDAO**

**Na Peter Orwa**

BADO ni wiki ya mageuzi makubwa ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ikitawaliwa na kishindo cha nafasi ya makamu mwenyekiti kupeana wazee na magwiji wawili, Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, kupokea kijiti cha Mzee Philip Mangula.

Hadi sasa, CCM ni kati vyama ambavyo vinadumu madarakani barani Afrika kutoka historia ya kupatia nchi zao ukombozi kutoka kwenye ukoloni.

Ikiulizwa kwanini? Hiyo ni mada ngumu ambayo inaamsha ubishani mkubwa mithili ya anayethubutu kufukua hoja ya ustadi linganifu uwanjani katika soka la vilabu vya Simba na Yanga.

Mchambuzi wa habari, Gwandumi Atufwene Mwakatobe muda mfupi baada ya kutangazwa Kinana, Makamu Mwenyekiti mpya wa CCM (Bara), alipohojiwa na chombo kimoja cha kimataifa kuhusu sababu ya kinachoiwezesha CCM kudumu madarakani akajibu ni 'mabadiliko' kulinganisha na vyama vingine, viongozi wake wanadumu sana.

Hata hivyo akawa na lake kulalamika kwamba 'vijana hawapewi nafasi.' Katika ujumla ikiiangaliwa staili ya CCM inatumia ilichorithi toka kwa TANU na kabla ya hapo, TAA, zikiwapo mbinu kuu tatu.

Mosi, inatumia urafiki na makundi ya kijamii ikiwa na mwenendo wa kuwanasa na kuwaumba wanachama; pili inajenga muundo wa kitaasisi wa kufanya kazi; njia ya tatu imekuwa ikijenga mtandao unaozama mbali na maeneo mengi ukiimarisha wananchi waliko kupitia matawi na wanachama.

Daima haijawahi kuyaacha hayo ambayo ni zao la moja kwa kazi iliyofanywa na Mwalimu Julius Nyerere.

Akiwa katika mkakati wa kusaka uhuru tangu kuzaliwa TANU, Mwalimu Nyerere alijipenyeza sana katika makundi ya kijamii, hasa akigawanya katika sura kuu; wanawake, vijana, wazee; na vyama vya wafanyakazi.

> Wafanyakazi nao wakawa sehemu ya siasa za TANU hata baada ya muda mfupi Kawawa akaingia rasmi katika nyendo za TANU kusaka uhuru, alikodumu nao miaka yote.

Kinamama kihistoria wamekuwa mtaji mkubwa wa katika siasa za CCM tangu zama hizo TANU ilipojenga urafiki na kinamama wapika pombe Kariakoo Dar es Salaam, akakutana na Bibi Titi Mohamed aliyewakusanya wenzake kwa mafaniko makubwa hata baada ya uhuru.

Kuna wakati, TANU ilitumia kundi hilio kufikisha siasa zake katika maeneo ilikopigwa marufuku, mfano katika baadhi ya wilaya za mkoani Tanga.

Vivyo hivyo, ufafanuzi huo unafanana na aliyonipa Mzee Rashid Kawawa miaka 20 iliyopita, kwamba Nyerere aliponogewa na msukumo mkubwa wa Shirikisho la Wafanyakazi Tanganyika (TFL), akaomba ubia kutoka kwa Katibu Mkuu, Kawawa.

Wafanyakazi nao wakawa sehemu ya siasa za TANU hata baada ya muda mfupi Kawawa akaingia rasmi katika nyendo za TANU kusaka uhuru, alikodumu nao miaka yote.

Pia, nikapata simulizi kama hizo kutoka kwa Mama Maria Nyerere, nilipomhoji kijijini Butiama, naye akanidokeza mtaji wa kisiasa wa kundi la vijana na kwa namna ya kipekee kuifikia jamii.

Anasema, TANU ikawa rafiki na klabu ya soka ya Yanga iliyotumika vyema kuwa kichaka kuunganisha vijana kwa shinikizo la uhuru, Mratibu Mkuu akiwa mdogo wa Mwalimu, Marehemu Joseph Nyerere. Ndio maana haishangazi Yanga sasa ikijiita 'timu ya wananchi.'

Eneo lingine ni kundi la wazee ambalo kwa kiasi kikubwa Mwalimu Nyerere aliratibu mwenyewe, wakimpa njia na miongozo kufanikisha mkakati yake, ikiwamo maeneo kama Bagamyo akikutana na magwiji wake waliomsaidia kama vile Sheikh Takadiri.

Hata baada ya uhuru, TANU iliendeleza urafiki na makundi hayo kwa kuzindua jumuiya rasmi kama sehemu yake, kudumisha ushirikiano huo. Hata hivvo, ililalazimka kuiengua Jumuiya ya Wafanyakazi, baada ya kuingia mfumo wa vyama vingi vya siasa, mwaka 1992.

Hata hivyo, ikiangaliwa nje ndani, CCM haijawahi kujiweka mbali katika urafiki wale na jumuiya ya wafanyakazi na hadi sasa ikidumisha unasaba wao kihistoria, ikitiliwa maanani nao wanabeba kundi kubwa katika jamii.

Mpaka sasa kupitia kauli ya aliyekuwa Katibu Mkuu Yusuf Makamba, bado wanaendeleza ushoga na kundi la kinamama kwa kuwa ndio wabia wakuu na waaminifu kuwapatia ushindi, kwani ni wepesi kuungana na waaminifu.

Katika ufafanuzi wake, aliwaainisha kinamama kwamba wafikapo kwenye uchaguzi wa kile waliochokiahidi huwa wanakitimiza, tofauti na wanaume ambao mara zote ni wa kusimamiwa, maana wanaweza kubadilika njia panda, wanapopata ushawishi mpya, ushahidi ukionekana kwa makada waandamizi wa vyama vya siasa na hasa vipindi vya uchaguzi.

Zao la yote TANU hadi baadaye CCM imeendelea kujichimbia mtandao wa kina, kulingana na sera na wakati unaohitajika, muda wote inathamini matawi na nyenzo na propaganda zake, huku timu ya wazee muda wote inabaki kuwa mlezi, mlinzi na mshauri mkuu wa chama.

**UUMBAJI MAKADA**

Tangu zama za TANU wanachama wapya baada ya kunaswa, walisukwa na kuingiziwa falsafa na itikadi na waumini wa chama, kabla ya kupewa majukumu ya ndani. Haikuwa tofauti sana na mbinu zitumiwazo kidini.

Kwa walioandaliwa kuwa viongozi walisukwa kupitia kilichokuwa chuo chake maalum, Kivukoni Dar es Salaam (sasa Mwalimu Nyerere Academy), hata ikawafanya wengi waliopewa nafasi iwe katika chama au serikalini, tayari walishanolewa.

Pia kuna njia ya pili TANU ilitumia kupenya kwenye nguzo ya wasomi walikowashawishi kujiunga nao kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakiwasuka huko huko chuoni na badala ya kuingia katika ajira, wao walichukuliwa katika chama.

Ni staili hiyo iliyokuwapo zama hadi miaka ya 1970, ilitumika wakianza na kujitolea katika chama, wakaajiriwa na baadhi wakapelekwa jeshini kusukwa chuoni Monduli kuimarishwa kwa ukakamavu, stadi za kiaskari na falsafa ya kijeshi "utii na nidhamu."

Hapo ndipo kuna majina kama Luteni Kanali Jakaya Kikwete, Kapteni Ukiwaona Ditopile Mzuzuri na Kapteni George Mkuchika.

Hiyo ni mbali na waliopitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mujibu wa sheria, wahitimu wote wa kidato cha nne na kupata mafunzo ya mwaka mmoja na zaidi.

**MUUNDO WA CCM**

Mtaji mwingine ambao TANU hadi CCM imeiwekea maboresho yasiyotetereshwa, ni kuwa na sura inayogawanyika katika maeneo makuu matatu.

Nguzo zenye uamuzi mkuu ndani ya CCM, kama vile Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, huwa hazikosi wazee wenye kuijua chama kwa kina, wazalendo na wana historia nayo ndefu.

Kwa miaka yote hata katika ngazi ya Sekretarieti ya Utendaji chini ya Katibu Mkuu, ni miaka mingi imedumu na wakongwe wenye historia ya chama, wakiendesha gurudumu lake la kila siku. Hao wana mchango mkubwa kukabili kasoro za ndani.

Hiyo inaanza na nafasi ya Mwenyekiti, inayoendana na anayepewa uongozi wa Rais, kwa mujibu wa mchujo wa CCM, kama si mzee kiumri, bado busara na weledi wake zimefika ngazi ya uzee na ana washauri wa kutosha.

Pia wanamfuatia kiutendaji, itakumbukwa, kuanzia Katibu Mkuu wa Kwanza, Mzee Rashid Kawawa, akichukua kiatu cha mtangulizi, Katibu Mtendaji Pius Msekwa. Kuna wengine kina Dk. Lawrance Gama, Philip Mangula, Wilson Mukama, Yusuph Makamba na Kanali Kinana wameiva kiumri na uzoefu.

Hiyo ni hali iliyoendana na timu inayounda sekretarieti ya utendaji, kuanzia wakuu wa idara walikokuwapo magwiji, kwenye idara zake kama Oganizesheni, Mipango na Uchumi, pia Itikadi na Uenezi, hali kadhalika kuwa watendaji wakongwe, kama vile kina Marehemu Mzee Mwasamale.

**INAENDELEA UK. 14**

MIAKA 100 YA MWALIMU NYERERE

# Makomredi Mangula, Kinana, uzao wao unadumu kwa kuilinda CCM

**Na Peter Orwa**

WIKIENDI iliyopita umma umeshuhudia jambo jipya ndani ya uongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kupata makamu mwenyekiti mpya (Bara), Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, anayepokea kijiti kutoka kwa mtangulizi anayepumzika, Philip Mangula, jiji la Dodoma likitikisika.

Kama ilivyo ukubwa wake CCM, ni tukio lililochukua sura pana kitaifa, maana majina yenyewe makubwa na walioratibu tukio wazito, wakiongozwa na mwenyekiti wa chama, Rais Samia Suluhu Hassan.

Mara moja baada ya matokeo kutangazwa kuanzia ulingo wa habari nyumbani hadi kimataifa kukasikika mijadala yenye hoja hasi na chanya. Kama wanenavyo wataalamu wa siasa za Afrika huwa wanajadiliwa wanasiasa kuliko vyama vyao, kwa lililo chanya hata hasi.

Kanali Kinana na kaka yake aliyemzidi kwa miaka 10, Philip Mangula wana sifa zinazofanana katika baadhi ya maeneo, wote walishakuwa makatibu wakuu kwa vipindi tofauti wakiacha rekodi na wanakijua chama ndani nje.

Hulka zao ni wakimya, ila inaporejewa kuifanya kazi wana uelediuliotukuka, lakini kikubwa wote kifalsafa ni watendaji zaidi kuliko kauli na kiitikadi ni wajamaa kindakindaki.



Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### YAKE AFANDE KINANA

Kinana ameshiriki sana kuratibu kampeni za Uchaguzi Mkuu wa CCM, ikiondoka na sanduku la ushindi.

Ana historia ndefu jeshini alikotumikia miaka 20, akigota na cheo cha kanali, kinachompa sifa kijeshi kuongoza timu ngazi ya kambi.

Huko akang'atuka baada ya mabadiliko ya nchi kuingia vyama vingi vya siasa mwaka 1992, kwa askari walitakiwa kuamua, ama kubaki jeshini au kuwa nje kwa wanaotaka kuegemea siasa, yeye akanyosha mkono awe nje ya jeshi.

Darasani nako 'hajambo'. Ana shahada ya sanaa akizama katika Siasa na Ushirikiano Kimataifa, kutoka chuo kikuu cha nchini Yugoslavia, pia Shahada ya Uzamili katika Menejimenti na Utawala wa Umma, kutoka chuo kikuu maarufu duniani cha Harvard, Marekani.

Tayari Kinana alishashika nafasi za juu za uongozi kisasa akiwa naibu waziri katika wizara mbili tofauti, zote zenye uhusiano wa moja kwa moja na fani zake.

Pia, ameshakuwa Mbunge wa Arusha Mjini kwa misimu miwili, Spika wa Bunge la Afrika Mashariki kabla ya kurejea kutumikia chama chake, ikiwamo kuratibu kampeni na baadaye kuwa mtendaji mkuu, kwa maana ya Katibu Mkuu wa CCM.

Wikiendi iliyopita akiwa katika maisha ya kustaafu, akajikuta kwenye wito wa chama na hadi kujikuta tena anaweka rekodi mpya anayotakiwa mwanasiasa au chama kuwa nayo, 'kukubalika' au wataalamu wa sayansi siasa wanaita 'Political Legitimacy.'

Kanali Mstaafu Kinana, ameneemeka na hilo alipozoa kura asilimia 100 kutoka kwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM, jijini Dodoma, baada ya jina lake kupendekezwa.

Naye kwenye hotuba yake kushukuru akiwa kwenye hulka yake ya upole na mtulivu, akaahidi dira yenye mambo kadhaa ikiwamo, kutenda haki, demokrasia ya kweli katika chama na kumwakilisha kwa nguvu kubwa mwenyekiti wake, Rais Samia.

Hapo kila mwisho, akahalalisha hoja yake akinukuu Katiba ya CCM, kuwa ndio wajibu mkuu wa Makamu Mwenyekiti, akaiambatanisha na darasa kwa wanachama kuwa 'hakuna mwenye CCM.'

### KOMREDI MANGULA JE?

Kama ilivyo kwa Kinana, anayeondoka Mzee Mangula ana safari ndefu katika chama, hulka ya ukimya sana huku akili yake ikifanya kazi ya ziada kwa wajibu mbele yake.

Binafsi, nafasi pekee ambako nimemuona amelazimika kufanya hivyo ni kwenye mikutano ya hadhara ya siasa.

Nakumbuka wakati fulani nilikuwa na miadi ya kuzungumza naye ofisini katika jukumu langu la ki- unahabari. Ni bahati mbaya ahadi zetu hazikutiamia mara tatu, kutokanma na mwingiliano wa ratiba ofisini kwake, Mtaa wa Lumumba, katikati ya Dar es Salaam.

Hata hivyo, kilichonishangaza, akiwa juu kwangu kiumri, mamlaka kikazi, nafasi ya uongozi dhidi yangu, ndiye alikuwa chini kuniomba msamaha.



Mzee Philip Mangula.

Nasema, ilinishangaza kwa sababu uhalisia tunaokutana nao katika fani ni tofauti. Akapendekeza mbadala iwe siku ya mapumziko Jumamosi nyumbani kwake Oystebay (kama nakumbuka vizuri Mtaa wa Mahenge Lane), maana yalikuwa mazungumzo ya kina.

Siku ilifika tukakutana naye, ambako nikashuhudia mapya zaidi. Akanikaribisha katika mazungumzo ya faragha barazani kwake penye mandhari nzuri na tukiwa tunaendelea, nikashuhudia inavyonenwa "utamuona kwa maneno na matendo yake."

Mangula katika shati lake la kitenge la mikono mirefu staili inayopendwa sana na wanamapinduzi na wanaharakati wa Kiafrika, akaniandalia kinywaji soda tulichokunywa kijamaa, kwa mtindo chupa moja kwa glasi mbili kila mmoja na yake, huku tikiendeleza mazungumzo. Mara zote akilazimisha kunimiminia, japo sikupenda kuona namvunjia heshima.

> "Mara nyingi kikazi nikawa nawasiliana naye hasa panapokuwapo makubwa yanayoamuliwa na CCM, yeye mtendaji mkuu nilipenda kupata ya kina kwake na daima akanipatia nafasi hiyo ya ufafanuzi wa kina.

Ni falsafa iliyonikosha sana ikinionyesha kiasi ustaarabu na ujamaa umemkaa. Ni mtindo wa maisha niliyopkutana nayo kabla kwenye mazungumzo kama hayo na marehemu Balozi Mhina, aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma (awamu ya kwanza), nyumbani kwake Makongo Juu, Dar es Salaam, tukichangia soda chupa moja kwa glasi mbili.

Naye mwana - itikadi huyo wa Ujamaa, akanitambulisha rafiki yake ambaye baadaye akawa Rais wa Msumbiji, Samora Machel, walishibana hata akapatiwa kombati za Frelimo, akimuita kwa jina Kamarade (Komredi Mhina).

Nilichobaini kwa Mangula, hakupenda kutumia nafasi yake kuwa juu ya mwingine kumdhalilisha hata akiwa mdogo, huku akiwa na tabia ya kumsoma mtu mantiki, busara na weledi wake katika jambo, akibaki ndani ya upole wake.

Mara nyingi kikazi nikawa nawasiliana naye hasa panapokuwapo makubwa yanayoamuliwa na CCM, yeye mtendaji mkuu nilipenda kupata ya kina kwake na daima akanipatia nafasi hiyo ya ufafanuzi wa kina.

Mojawapo ilikuwa baada ya mazungumzo naye ofisini kwake yaliyochukua wastani dakika 45. Nilipomaliza akaniuliza kwa kauli ya chini "Je, una diary?" Nikamjibu 'sina', huku nikipata shida kutafsiri mantiki ya swali lake, maana ilishafika mwezi kama huu.

Hapo akanyanyua 'diary' mezani na kunipatia 'chukua hii.' Nilisita kupokea, nikimjibu ahsante! Lakini, ghafla nikahimizwa kwa staili ya kushambuliwa na wasaidizi wake, lakini kwa ishara ya mazuri, chukua!

Hao ni Katibu wake, marehemu Gordon Mwakitabu na aliyekuwa na Ofisa Habari, Thobias Mwilapwa. Ndipo kichwa kikanifunguka, ina salamu ya mema na heshima kwangu.

Baadaye wakanipigia simu kwamba 'dairy' ile ina tafsiri kubwa sana, kwani hawajamuona mwanahabari akipewa hilo, nami nikapata tabasamu la moyoni, nikiongeza darasa Mangula ni nani kifalsafa.

Uamuzi wangu nikaitunza 'diary' ile muongo mmoja na nusu hadi mwaka huu nilipompatia mwanangu kwa salamu zetu kupongezana, nikimulezea sijatumia hiyo miaka yote (16), pia nikimuelimisha imetoka kwa mtu wa namna gani, apate mantiki ya zawadi hiyo na maandishi 'live' ya Mzee Mangula kitabuni kutoka 2005.

Hata wikiendi iliyopita nikiwaona wanapokezana majukumu ya CCM, napata majibu zaidi kutoka gizani, uzao uliopikwa mkononi mwa Mwalimu Nyerere, sasa unafanya kazi yake.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Mwafrika wa kwanza kuongoza ILO

**Na Christina Mwakangale**

NI karne moja kwa Shirika la Kazi Duniani (ILO), likiadhimisha karne hiyo na historia imewekwa mwaka huu, baada ya Gilbert Houngbo, Mwafrika kutoka Togo, kuchaguliwa kuliongoza.

Gilbert Houngbo (61), Mkurugenzi Mkuu wa ILO, atakayeanza kuwajibika Oktoba Mosi mwaka huu, baada ya mkuu wa sasa Guy Ryder raia wa Uingereza kumaliza muhula wake.

ILO iliundwa mwaka 1919 shughuli zake, kutazama mwelekeo wa kazi duniani na changamoto. Houngbo, ana mengi ya kujikita kwenye sekta hiyo hususan katika bara la Afrika.

Mashirika ya kimataifa kuanza kushikiliwa na Waafrika imeanza kuonekana hivi karibuni, bila kumsahau Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), Ngozi Okonjo-Iweala.

Houngbo ameshika nyadhifa tofauti nchini Togo, alikuwa Waziri Mkuu, kuanzia Septemba mwaka 2008 hadi Julai 2012.

Anachukua nafasi hiyo, baada ya awamu mbili za upigaji kura kisha bodi inayoongoza shirika hilo kumchagua kumrithi mwanaharakati wa vyama vya wafanyakazi wa Uingereza, Guy Ryder, anayehitimisha miaka 10 kuongoza ILO.

Houngbo, hivi sasa ni Mkuu wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), wenye makao yake makuu jijini Roma, Italia, alikuwa miongoni mwa wagombea watano.

Awali alipewa nafasi kubwa kushinda uchaguzi huo, kutokana na kuungwaji mkono mkubwa na wafanyakazi pamoja na Umoja wa Afrika (AU).

### MCHAKATO WA UCHAGUZI

Wapinzani wa Houngbo katika kinyang'anyiro hicho walikuwa Waziri wa zamani wa Kazi wa Ufaransa, Muriel Penicaud, Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje wa Korea Kusini, Kang Kyung-wha, mjasiriamali kutoka Afrika Kusini, Mthunzi Mdwaba na Naibu Mkuu wa ILO anayetoka Australia Greg Vines.



Gilbert Houngbo (61), Mkurugenzi Mkuu wa ILO, atakayeanza kuwajibika Oktoba ijayo. **PICHA: MTANDAO**

> Alihamia nchini Canada mwaka 1983 na alikohitimu Shahada ya Uzamili ya Uhasibu na Fedha.

Ushindi wa Houngbo, unaashiria mabadiliko makubwa kwa ILO, ambayo tangu kuanzishwa kwake mwaka 1919, limekuwa likiongozwa na kutoka Ulaya au Amerika pekee.

Shirika hilo kongwe zaidi la Umoja wa Mataifa (UN), lina nchi wanachama 187 na wajumbe 56 katika baraza la uongozi, huku nusu yao wakiwakilisha serikali na waliosalia wakiwakilisha waajiri na wafanyakazi.

### HOTUBA YA USHINDI

Katika hotuba yake baada ya upigaji kura, Houngbo alipongeza hatua za mchakato mzima wa uchaguzi, akisema matokeo ya uchaguzi yana ishara nyingi, ikiwamo kutimiza matarajio ya kijana wa kiafrika ambaye malezi yake ya unyenyekevu yaligeuka mafanikio ya haki kwa jamii.

Awali mkuu wa sasa, Guy Ryder akizungumza katika baraza lililoongoza uchaguzi huo, alimsifu Houngbo kwa kuweka historia na aliona ni heshima muhimu.

Houngbo, anakabiliwa na changamoto za rekebisho ya kanuni za shirika hilo zinazoshughulikia masuala ya ajira duniani katika kipindi ambacho mabadiliko ya teknolojia yanashuhudiwa kwa kasi.

Gilbert Fossoun Houngbo, amezaliwa Februari 4 mwaka 1961, na amekuwa mwanasiasa na mwanadiplomasia, aliyeshika nyadhifa tofauti UN, Shirika la Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), ofisi ya ILO na IFAD.

Houngbo, amezaliwa vijijini huko akiwa mtoto wa 11 kati ya 18 ana Shahada ya Utawala wa Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Lomé kilichopo Togo.

Alihamia nchini Canada mwaka 1983 na alikohitimu Shahada ya Uzamili ya Uhasibu na Fedha.

Houngbo, alipata uraia wa Canada na kufanya kazi Price katika asasi ya kifedha ya Waterhouse, jijini Canada, pia ni mwanachama wa taasisi ya kifedha Canadian Institute of Chartered Accountants.

Katika hali tata, Septemba 7 mwaka 2008, Rais wa Togo, Faure Gnassingbé alimteua Houngbo kuwa Waziri Mkuu wa Togo, akichukua nafasi ya Komlan Mally, ambaye alijiuzulu.

Uchaguzi wake ulibainishwa kwamba Houngbo ni mtu wa maafikiano ambaye angewezesha maridhiano ya kitaifa. Baadhi ya waangalizi walihusisha uteuzi wake na nia ya kuboresha taswira.

Wakati Katibu Mkuu wa UN zamani akiwa Ban Ki-moon September 11 mwaka 2008, Houngbo na kiongozi huyo na amepongezwa hatua za mafanikio UNDP.

Siku chache baadaye serikali ya Togo ikaundwa Septemba 15, mwaka 2008 ikiwa na mawiziri 27.

• ***Kwa mujibu wa Mtandao.***

# Karata kuu tatu zinazobaki mtaji wa CCM, wazee rasilimali kuu

**INATOKA UK. 12**

Hiyo ni hali iliyoendana na timu inayounda sekretarieti ya utendaji, kuanzia wakuu wa idara walikokuwapo magwiji, kwenye idara zake kama Oganizesheni, Mipango na Uchumi, pia Itikadi na Uenezi, hali kadhalika kuwa watendaji wakongwe, kama vile kina Marehemu Mzee Mwasamale.

Mabadiliko yalianza kushuhudiwa katika uongozi wa serikali ya awamu ya tano, pale alipoteuliwa Katibu Mkuu, Dk. Bashiru Ally ambaye ana sura ya ujana, hakutokea kwenye kapu la malezi ndani ya CCM, ila kwa sura ya pili ni mweledi wa sayansi ya siasa na utawala kwenye fani yake.

Moja ya karata zilizompa baraka, ni pale alipokabidhiwa jukumu maalum, ikiwamo kuongoza tathmini mali za chama kitaifa, akalifanikisha.

Vivyo hivyo, ndivyo alivyo Daniel Chongolo, ambaye utumishi wake katika fani yake ya uanahabari alihudumu kwenye chombo cha CCM, kisha akahamishiwa kwenye sekretareti ya chama, kabla ya kuwa mkuu wa wilaya, hadi nafasi ya sasa.

Kiumri hakukuta utaratibu wa kupeleka mafunzoni Kivukoni yameshapita, ingawa sehemu ya kazi alikoanza nazo ni kuzindua chuo kama cha Kivukoni cha CCM.

### VIJANA NA CCM?

Hapo ndipo inaoibua hoja pale watu wakashangaa vijana kupewa ukatibu mkuu CCM, kwani wamezoea ni nafasi ya magwiji wazee wakongwe huku sasa sekretariti yake ikiwa na wa umri wa Dk. Bashiru na Chongolo au kidogo.

Hapo inaleta jibu kwa mchambuzi Gwandumi, kuhusu 'vijana hawapewi nafasi CCM?' Ni sera anazoziendeleza Rais Samia Suluhu Hassan, kwamba ni wakati wa kuwapa nafasi vijana katika Baraza la Mawaziri lililoko sasa kuwa na vijana zaidi.

Hata hivyo ikiangaliwa 'kwa miwani' CCM badio iko palepale katika falsafa yake ya asili, kwamba nafasi ya ulezi kiutawala mithili ya Bodi ya Wakurugezi kwenye mashirika inabaki kwa wazee. Hapo ndio unamuona mwenyekiti ana miaka inayoelea kwenye 60 na makamu aliyeondoka, kwenye umri wa miaka 80 akimwachia aliyeko kwenye 70.

Fursa na hulka yao, inaweza kuangaliwa kwa angalizo la Mzee Yusuph Makamba mwenye miaka 85 aligawa maneno ya hekima yakiwa wamenakishiwa na maneno ya busara kuiweka sawa CCM, kikao kilichomrejesha nyumbani kada maarufu – Bernad Membe; bila shaka ni kupitia jitihada wazee.

Leo hii wakitajwa makada walioshamiri kupitia Umoja wa Vijana CCM (UVCCM), kuna mkono mkubwa wa makada walezi wazee.

Mwanasiasa na kada maarufu, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, katika mazungumzo naye mwaka 1999, akitwaa uenyekiti wa UVCCM, aliniambia ni zao la Mzee Philip Mangula.

Kwa vipi? Anafafanua, utashi wake kisasa ulianza wakati huo wakiishi katika Chuo cha CCM Kivukoni, baba yake akiwa mkuu wa chuo na Mangula alipokuwa mkufunzi, anaukumbuka wimbo wa chama anaonukuu "Eeeh vijana, vijana vijana tayari…"

Nchimbi huyo bado akang'ara kitaifa akiendekezea siasa hizo hadi alikokuwa chuoni, IDM Mzumbe, Morogoro alikokuwa kada aliyeiva na wenzake kama vile Amos Makala, aliye hazina kubwa ya kisiasa na utendaji.

Hapana shaka, hiyo ndio sababu ya Kanali Mstaafu Kinana kupewa rungu akiwa na miaka 70 kumsaidia Mzee Mwenziwe, Rais Samia na hilo sio geni, kwani hata Rais Nyerere, alipostaafu uongozi wa chama na kisa uenyekiti, alimwachia mzee mwenziwe Kawawa akiiangalia kwa nafasi makamu mwenyekiti.

Wote walipostaafu kufuatilia chama chao hata wakawa nje, bado mlolongo wa makamu mwenye na hasa bara, uliendelea na wazee kama kina John Malecela na Pius Msekwa.

Hata ikiangaliwa mbinu mkakati za chama kama CHADEMA, nacho sasa kinamega mbinu mkakati za CCM, ikiwekeza zaidi kwa vijana na kinamama.



# Jumuiya yatakiwa kushirikiana na serikali kutatua migogoro

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Maridhiano Taifa, Shekhe Mussa Salum, amewataka viongozi wa jumuiya hiyo kufanya kazi kwa pamoja na serikali ili kutatua migogoro inayojitokeza pamoja na kukemea vitendo vya kikatili.

Shekhe Salum aliyasema hayo kwenye mkutano wa viongozi wa mikoa na wilaya wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania uliofanyika mkoani hapa.

Alisema kuwa wao kama viongozi wa ngazi za mikoa na wilaya pamoja na majukumu waliyonayo pia wahakikishe wanafanya kazi kwa kushirikiana na serikali kushughulikia migogoro mbalimbali na kukemea vitendo vya kikatili vinavyojitokeza.

Alisema lengo la Jumuiya hiyo ni kuhakikisha amani, upendo umoja na mshikamano unadumishwa na watu wake wanaishi kwa utulivu.

"Hapa ninaomba niwahakikishie kuwa chombo hiki cha Jumuiya ya maridhiano kinatambuliwa na serikali, hivyo ninawaomba mjiamini kuwa nyinyi ni sehemu ya kuhakikisha amani na utulivu unakuwapo hapa nchini," alisema.

Hata hivyo, aliwataka viongozi hao kuhakikisha wanashiriki katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo ili kujiinua kiuchumi.

"Mnapokuwa kwenye maeneo yenu mhakikishe wanajishughulisha na fursa mbalimbali zinazojitokeza, ikiwamo kujenga mahusiano ya karibu na wadau badala ya kusubiri kuwezeshwa na ofisi yenu hii ya Jumuiya ya Maridhiano," alisema.

## Asakwa tuhuma za kumlawiti mwanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linamtafuta mwanamume mmoja anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka kati ya 35-40 kwa tuhuma za kumlawiti mwanafunzi wa kidato cha kwanza.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Onesmo Lyanga, alisema tukio hilo lilitokea Aprili mosi, mwaka huu saa 6:00 mchana katika Bwawa lililopo mtaa wa Senje Kata ya Msalato jijini hapa.

Alisema mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo baada ya kuwakamata wanafunzi watatu waliokuwa wakichota maji kwa ajili ya usafi wa darasa na kuwatishia kuwaua kwa panga kisha kumlawiti mmoja wao.

"Walikuwa wafunzi sita wameenda kuchota maji katika hilo bwawa. Na wakakutana na mtu mmoja ambaye wao wanamtambua kwa sura na waajiri wake. Mtu huyo aliwatolea vitisho na kuwauliza maswali, kwanini wanateka maji hapo."

"Na akawauliza wale ambao ni mara yao ya kwanza kuteka maji katika bwawa hilo. Wakatokea wanafunzi watatu wakamjulisha kwamba wao ni mara yao ya kwanza akawaambia nyinyi nendeni."

"Lakini akawachukua wanafunzi watatu, na inasadikiwa alikuwa na kitu kama panga na kuwatisha na kuwachukua kuendelea kwenda katika hivyo vichaka, ndipo huko alipomlawiti mwanafunzi mmoja kati ya hao watatu," alisema.

Aidha, Lyanga alisema mwanafunzi huyo anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

"Uchunguzi unaendelea wa kumtafuta mtuhumiwa na kumbaini, lakini naagiza ajisalimishe haraka kwa kuwa anatambulika kwa sura," alisema.



Rais Samia Suluhu Hassan (kulia), akikabidhiwa bidhaa ya mchele ya 'Pure Aromatic Rice' na kampuni ya Raphael Group, alipotembelea banda la Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) katika hafla ya uzinduzi wa ugawaji wa vitendea kazi kwa maofisa ugani kilimo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 'Wasambazaji mbegu watoe elimu kwa wakulima'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Siza Tumbo, amewataka wasambazaji mbegu kwa wakulima kuhakikisha wanatoa elimu ya matumizi ya mbegu kwa wanunuzi ili kuongeza watumiaji wa mbegu bora zinazosambazwa na Wakala wa Mbegu nchini (ASA).

Akizungumza wakati akifunga kikao baina ya ASA na wasambazaji walioingia mkataba wa kusambaza mbegu na Wakala huyo, Prof. Tumbo, alisema takribani asilimia 10 ya wakulima wanatumia mbegu bora ambazo zimeboreshwa.

"Wasambazaji wa mbegu mnapaswa kuwa maafisa ugani kuwaelimisha wanunuzi umuhimu wa matumizi ya mbegu bora, jambo litalochangia kuongeza uzalishaji wenye tija kwa wakulima kwa kutumia mbegu bora za mazao."

"Ni asilimia chache ya wakulima wanaotumia mbegu bora za ASA, hivyo mnapaswa kuongeza bidii ya kutawanya mbegu kwa wakulima pamoja na kuwapa elimu ya kuzitumia," alisema. Akizungumza kuhusu uzalishaji wa mazao wenye tija ambao utaleta matokeo chanya, alisema mkulima anatakiwa kuwa na viuatilifu, mbolea, mbegu bora na vitu vingine ambavyo vitamsaidia kuboresha shamba lake kabla na baada ya msimu wa mavuno.

"Mpaka leo hii bado wakulima wanahangaika na uzalishaji wa mahindi kutokana na kutofuata taratibu za kilimo bora kitendo kinachochangia kupata tani chache za mahindi kwa heka moja ya shamba, ukilinganisha na mkulima anayetumia kilimo bora," alisema.

Alisema wakulima wakizingatia kufuata kanuni za kilimo, watasaidia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu bora ambazo zitaleta tija kwa taifa.

Naye, Mtendaji Mkuu wa ASA, Sophia Kashenge, alisema maelekezo waliopewa na wizara watayafanyia kazi kikamilifu ikiwamo kuhimiza wadau wasambazaji wa mbegu katika maeneo ya pembezoni kuongeza bidii ya kuwafikishia wakulima kwa wakati mbegu.

Alisema moja ya kero inayowasumbua wakulima ni ucheleweshaji wa mbegu, hilo watalifanyia kazi ili kuhakikisha wanaboresha.

"Tunashukuru serikali kwa kuamua kufanya kazi kwa karibu na sekta binafsi, hili litaongeza ufanisi katika usambazaji wa mbegu," alisema.

Alisema watahakikisha wanaongeza upatikanaji wa mbegu bora ili wapate kwa wakati kwenye msimu wa kilimo.





# Mbaroni tuhuma mauaji ya mumewe

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia Riziki Henry (22), mkazi wa Nditu wilayani Rungwe kwa tuhuma za mauaji ya mume wake, Ayubu Aron (33).

Riziki anadaiwa kumua mume wake kwa kumpiga na kitu butu kichwani kisha kumchoma na kitu chenye ncha kali kisogoni baada ya kuulizwa sababu za kurudi nyumbani usiku.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema jana kuwa tukio hilo la mauaji lilitokea Aprili 2, mwaka huu, majira ya saa 9:00 alasiri katika kijiji cha Nditu. Mtuhumiwa anadai kuwa baada ya mke wake kurudi nyumbani usiku, kulitokea ugomvi uliosababisha mauaji.

Matei alisema baada ya tukio hilo, Aron alipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Rungwe ya Makandana kwa ajili ya matibabu lakini Aprili 2 majira ya saa 11:00 jioni alifariki dunia.

"Chanzo cha tukio hilo ni ugomvi uliotokana na mke wa marehemu ambaye ndiye mtuhumiwa kuchelewa kurudi nyumbani na alipoulizwa kwa nini amechelewa ndipo ulizuka ugomvi uliosababisha kifo cha mwanamume," alisema Kamanda Matei.

Alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Rungwe kwa ajili uchunguzi wa kitabibu.

Kamanda Matei aliongeza kuwa kutokana na tukio hilo, mtuhumiwa alikamatwa na kwamba upelelezi wa shauri hilo unaendelea na baada ya kukamilika, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nditu, Hostine Lupogo, alisema tukio hilo lilitokea Ijumaa Aprili 2, mwaka huu ambapo wenza hao walikuwa kwenye ngoma za asili.

Alisema wenza hao walikuwa wamelewa pombe na kwamba mwanamume ambaye ni marehemu kwa sasa, alitangulia kurudi nyumbani na baadaye mwanamke alirudi usiku na baada ya kuulizwa ulizuka ugomvi.

Baada ya kutokea ugomvi huo, alisema mdogo wa marehemu alikwenda kuamulia ugomvi huo pamoja na majirani wengine na kisha kuwaacha na kulipokucha asubuhi ya Jumamosi asubuhi, walifika nyumbani hapo kuwajulia hali ndipo wakaona mumewe hajaamka.

"Baada ya kugundua damu zinavilia kisogoni tulipiga simu kwa baba yake Aron na kisha kumpeleka kwenye zahanati ya Nditu lakini kutokana na hali yake wahudumu walimpa rufani hadi Hospitali ya Wilaya ya Rungwe Makandana ambako alifariki dunia wakati anapatiwa matibabu," alisema Lupogo.



Waziri Mkuu wa Burundi, Alain Guillaume Bunyoni (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Tanzania nchini Burundi, Dk. Jilly Maleko (wa tatu kulia), Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (wa pili kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (watatu kushoto), Mjumbe wa Bodi ya Benki hiyo nchini Burundi, Kahumbaya Bashige (wapili kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Burundi, Fred Siwale (kushoto) na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Burundi, Menard Bucumi, jijini Bujumbura nchini humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanahabari wawezeshwa mikopo kujikomboa kiuchumi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

CHAMA cha Wandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya (MBPC), kimeanza kwa vitendo kuwawezesha kiuchumi waandishi wa habari mkoani hapa kwa kuwapatia mikopo yenye riba nafuu.

Kwa kuanzia katika kipindi cha mwezi mmoja, MBPC imetoa mkopo wa zaidi ya Sh. milioni 3.2 kwa wanachama 15 ambao wamekopa kwa ajili ya kuanzisha biashara ndogo za kuwawezesha kujiingizia kipato.Akizungumzia mpango huo, Katibu wa MBPC, Kenneth Mwakandyali, alisema jana kuwa lengo la mpango huo ni kuwainua wanahabari wa mkoa wa Mbeya kiuchumi.

Mpango huo, alisema umeanzishwa mwaka huu kwa kuwaunganisha wanandishi wa habari ambao ni wanachama wa MBPC wenye nia ya kujikwamua kiuchumi na kuwahamasisha kuanzisha vikoba kama chanzo cha mapato ya fedha za kukopeshana.

Alisema kila mwanachama aliyejiunga ni vikoba alitakiwa kununua hisa moja kwa kima cha chini cha Sh. 5,000 kila wiki na mwanachama anaruhusiwa kununua kima cha juu cha hisa 20 kwa wiki ambazo ni sawa na Sh. 100,000 kwa wiki.

"Utaratibu huu ulituwezesha kukusanya zaidi ya Sh. milioni nne kwa Januari na Februari ambazo tuliona zinatosha kuanza kuwakopesha wanachama wetu wenye nia ya kuanzisha miradi midogo ya kujikwamua kiuchumi," alisema Mwakandyali.

Alisema utaratibu huo unawawezesha wanahabari kutoa riba kila wiki na kwamba mwisho wa mwaka kila mwanachama atapatiwa fedha zake ambazo alichanga pamoja na faida zilizopatikana kwenye riba yake ya mkopo.

Miongoni mwa wanufaika wa mpango huo, Nebart Msokwa, alisema kupitia mkopo huo, ameanza kuendesha shughuli za shamba na kumsaidia kununua mbolea, mbegu na kulipa vibarua.

Alisema chama hicho kimesaidia kubadilisha maisha yake na kuongeza juhudi katika kufanya kazi ili kupata fedha za kununua hisa na kulipa mkopo kwenye kikoba hicho cha Mbeya Press.

Mnufaika mwingine, Eliud Ngondo, alisema fedha hizo zimemsaidia kuendesha biashara yake ambayo kwa sasa imekuwa na ameongeza utoaji wa huduma.

Esther Macha, alisema mkopo alioupata ulimsaidia kulipa ada ya mwanawe anayesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kumwezesha kusoma kwa utulivu kuliko ilivyokuwa awali alipokuwa akipata usumbufu.

Kutokana na manufaa ya chama hicho, Macha aliwashauri wanahabari wa mkoa huo ambao hawajajiunga, kutumia fursa hiyo ili kujikwamua kiuchumi na kutimisa ndoto zao.

## Ukatili wa jinsia wakithiri Songwe

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

KESI 640 za vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake ziliripotiwa mkoani Songwe kati ya mwaka 2020 na 2021.

Katika kesi hizo kwa mwaka 2020 kesi za ukatili wa watoto zilizoripotiwa zilikuwa 324, zilizopata mafanikio ni 47 na zilizopo mahakamani ni 117.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Songwe, Atusungukye Dzombe, huku akibainisha kwamba kwa mwaka 2021, kesi zilizoripotiwa ni 316, kati ya hizo zilizofungwa ni 91, zilizopata mafanikio 44 na 134 zinaendelea na upelelezi.

Alisema takwimu hizo zinaonyesha kukithiri kwa vitendo vya ukatili mkoani hapa naq kwamba ili kukomesha vitendo hivyo, wameweka mpango wa kukabiliana navyo ili kutengeneza kizazi kinachodumisha haki na usawa.

Pia alisema mkoa umeanza kutoa elimu ya kupinga ukatili na athari zake nyumba kwa nyumba kwa kuwatumia maofisa kuanzia ngazi ya kata ambao wanawafikia ili kuwafundisha namna ya kuondokana na vitendo hivyo pamoja na kukabiliana navyo.

"Aidha tumeandaa kampeni ya kila wilaya kufanya matamasha ya kuhamasisha wananchi kupinga vitendo vya ukatili kama vile vipigo kwa wanawake,haki ya kumiliki mali, kumsomesha mtoto wa kike na kumpatia mahitaji yake pamoja na mimba na ndoa za utotoni," alisema Dzombe.

Alisema mkoa wa Songwe bado unakabiliwa na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na kwamba wilaya ya Mbozi ndio inaongoza kwa vitendo kama vile vipigo na manyanyaso mengine ambavyo huripotiwa katika ofisi yake na Dawati la Jinsia mara kwa mara.

Alizitaja baadhi ya sababu zinazochochea ukatili katika mkoa kuwa ni mila na desturi za kuoa wanawake wengi, hivyo wanaume wengi kuwaachia wanawake jukumu la malezi ya watoto, watoto wadogo kupelekwa kuchunga mifugo badala ya kupelekwa shuleni pamoja na wazazi kuwanywesha pombe watoto wadogo chini ya miaka mitano ili wapate usingizi wanapokuwa kwenye shughuli za shamba.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe , Omary Mgumba, alisema pamoja na serikali kujikita kujenga na kuboresha vituo vya afya, zahanati na hospitali, kuna baadhi ya watu hasa waishio vijijini kupeleka wajawazito kujifungua kwa wakunga wa jadi jambo ambalo uhatarisha afya mama na mtoto.

Alihamasisha jamii kuwapeleka wajawazito kwenye vituo vya kutolea huduma ili wapatiwe huduma bora za kujifungua ili kuokoa uhai wa mama na mtoto.



## Taasisi ya Karume kusaidia matatizo ya wazee

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia Zanzibar (KIST), Dk. Mahmoud Abdul-Wahab Alawi, amesema miongoni mwa malengo ya taasisi hiyo ni kuwa na ushirikiano na wazee pamoja na kujua matatizo waliyonayo.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wazee wanaoishi nyumba za Sebleni katika maadhimisho ya miaka 50 ya kumuenzi Rais wa kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume.

Alisema wazee wana mchango mkubwa katika nchi, hasa ikizingatiwa katika ujana walishiriki ujenzi wa nchi na kwamba ipo haja kuwalea na kuwatunza kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kuishi.

Alisema kwa mchango mkubwa walioutoa katika nchi, Taasisi ya Karume imeamua kumuenzi Rais huyo kwa kukabidhi misaada mbalimbali kwa wazee ikiwamo vyakula.

Mkurugenzi Alawi, alisema wamejipanga kutoa huduma mbalimbali katika nyumba wanazoishi wazee Sebleni ili kuwawekea mazingira mazuri yaliyowazunguka.

Akielezea huduma hizo ni za umeme, maji, vyoo pamoja na kuwapatia vyakula na mavazi.

Naye mlezi wa kituo hicho, Ashura Suleiman Juma, alisema anaishukuru taasisi hiyo kwa kuwapatia msaada mkubwa kwao na umefika kwa wakati kutokana na uhitaji wa huduma hizo.

Kwa upande wao wazee wanaoishi katika nyumba hizo walishukuru taasisi hiyo kwa msaada waliotoa kwa sababu wazee wana mahitaji mengi.

Maadhimisho ya miaka 50 ya kumuenzi aliyekuwa Rais wa kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume yaliandaliwa na Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kumuenzi Rais huyo, yaliyobeba kaulimbiu isemayo, "Sayansi na Teknolojia kwa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu".

# Makatibu wakuu waagizwa kusimamia fedha za miradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewaagiza makatibu wakuu kusimamia fedha za miradi ya ahueni ya UVIKO-19 ili kuhakikisha inakamilisha miradi hiyo kwa wakati.

Hemed aliyasema jana katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema serikali haitoridhia kuona miradi hiyo inavuka muda uliopangwa katika mikataba kwa kisingizio cha wakandarasi kuchelewa kupata fedha kwa urasimu wa watendaji wa wizara husika.

Alieleza kuwa fedha zimeshatengwa kwa ukamilifu ili kukamilisha miradi hiyo kwa lengo la kuwanufaisha wananchi wa Zanzibar.

Vile vile, alisema ni vyema kuepuka matumizi yasiyo na ulazima na fedha zitakazobaki zielekezwe katika miradi mingine kwa manufaa ya wananchi.

Aliwataka viongozi hao kuhakikisha wakandarasi wa miradi hiyo hawapati changamoto ya aina yoyote ili kuwarahisishia kazi zao kukamilika kwa muda uliopangwa.

Alikipongeza kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar kinavyoendelea na ujenzi wa madarasa katika mkoa huo na kueleza kuwa azma ya serikali ni kuhakikisha wakandarasi wazawa wanasimamia miradi hiyo kizalendo.

Kwa upande wake Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, Rashid Mzee Andallah, alisema ujenzi wa madarasa ndani ya Mkoa wa Kusini Unguja utakamilika kwa muda uliopangwa ili kutoa fursa kwa wanafunzi kukaa katika mazingira mazuri ya kusomea.

Alisema majengo hayo yanayojengwa na kikosi hicho atahakikisha yanamaliza kwa wakati na kwa kiwango cha hali ya juu ili kuondoa changamoto ya sehemu za kusomea wanafunzi wa mkoa huo na mikoa jirani.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid alisema Serikali ya Mkoa imefurahishwa kwa hatua iliyofikia miradi hiyo na kumuhakikishia kuwa viongozi wa mkoa huo wataendelea kusimamia miradi hiyo ili iweze kukamilika kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.



Waziri wa Utalii na Mambo ya kale Zanzibar, Simai Mohamed Said (katikati), akizungumza na wananchi wa Mji Mkongwe wa Zanzibar jana, wakati akisikiliza changamoto zinazo wakabili na kuzitolea ufumbuzi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# 'Bunge 'live' lisigeuzwe wabunge kujitafutia umaarufu'

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

CHAMA cha ADA Tadea kimesema kipindi cha runinga cha Bunge mubashara kitumiwe na wabunge kuleta manufaa, kutanua wigo wa demokrasia na kuelezea changamoto zinazowakabili wananchi badala ya matamshi hatarishi au wabunge kujitafutia umaarufu wa kisiasa.

Pia, wabunge wameshauriwa kutambua ndimi zao zenye maneno makali zinaweza kuwa bomu linaloweza kudhuru au kuiteketeza jamii.

Hayo yalielezwa na Naibu Katibu Mkuu wa ADA Tadea, Yussuf Mchenga, wakati akizungumza na Nipashe mjini hapa.

Alisema mamlaka za utawala kurudishwa kipindi hicho ni uamuzi sahihi na kuyageuza maudhui ya kipindi hicho kukiwa ndiyo mwanzo wa mabishano yasiyojenga hakutakuwa na maana.

Mchenga alisema chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, serikali yake imekusudia kubadili mwelekeo wa mambo hasi ili kuwa chanya na kufungua ukurasa mpya wa haiba ya maendeleo ya demokrasia, kukuza uhuru wa mawazo, kuzidisha uwazi na demokrasia shirikishi.

Alisema ni haki ya wabunge wa pande zote mbili, utawala na upinzani kushindana kwa hoja, kuchuana kwa kutumia uwezo binafsi na fikra anuai, lakini wasifikie mahali wakakosa simile na kujikuta wakitoa matamshi ya kutishia amani na utulivu wa taifa.

"Kipindi cha runinga 'bunge-live' kitumiwe na wabunge kuleta manufaa ili kutanua wigo wa demokrasia. Ikiwa kitatumika kinyume chake kwa kukamiana, kutoa matamshi holela au wabunge kujitafutia umaarufu wa kisiasa tutalikwamisha taifa letu," alisema Mchenga.

Alisema kazi ya kujenga taifa lenye umoja, mshikamano, utaifa na kuwafanya wananchi kuwa wamoja na uzalendo si jambo jepesi kama inavyofikiriwa na baadhi ya watu.

"Nilibahatika kuwa mmoja kati ya wabunge wa bunge maalum la katiba. Awali, bunge lile halikuwa na kanuni wala taratibu. Ilizuka mijadala mikali na majibishano ya kuogofya tukawa hatutambuani. Hata hivyo, nimsifu sana Spika Hayati Samuel Sitta, Naibu Spika, Ameir Pandu Kificho na Makamu Mwenyekiti, wakati ule akiwa Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Alisema, walitumia busara kubwa wakiongozwa na hekima na uzeofu katika mambo ya utawala hadi mambo yakakaa vyema na kuandika rasimu ya katiba mpya na bunge maalum la katiba iliokwamishwa na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa waliosusia.

"Ikiwa mbunge atakayesimama ili kuchangia hoja awe na nguvu ya hoja badala ya hoja zenye nguvu. Ni vyema taifa letu libaki kama lilivyo kuliko kuvurugwa. Hatuna mahali pengine pa kukimbilia zaidi ya Tanzania. Hata baada ya Bunge kumalizika Tanzania itabaki palepale," alisisitiza.

Hata hivyo, alisema Bunge ni la wananchi na wabunge wawakilishi wa watu na wananchi kuwasikia wabunge wao wanavyochangia hoja mbalimbali katika maendeleo ya kisekta ni jambo jema, lakini wasijisahau na kutaka kuugeuza ukumbi wa bunge ni eneo la kuvuruga maelewano.

HABARI KIMATAIFA



Rais Volodymyr Zelensky akiwa na wanajeshi wake. **PICHA: DW**

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# Russia yahojiwa vifo mji wa Bucha

• Wakimbizi wafikia milioni saba

**Kyiv,** UKRAINE

OFISI ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa imesema ushahidi kutoka Bucha unaonyesha kuwa vikosi vya Russia vililenga moja kwa moja raia.

Zaidi ya watu milioni 7.1 wamekimbia makazi yao kutokana na vita nchini Ukraine, kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamiaji (IOM).

Michelle Bachelet, Kamishna Mkuu wa Shirika la Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa, amesema idadi kubwa ni ya wanawake na wanachangia zaidi ya nusu ya waliolazimika kukimbia vita, shirika hilo limesema.

"Tumekuwa tukizungumza kuhusu uhalifu wa kivita katika muktadha wa kurusha makombora, milipuko ya mabomu na mizinga. Sasa wanahitaji kuchunguzwa. Lakini unaweza kusema kuwa kulikuwa na muktadha wa kijeshi, kwa mfano, kwa jengo lililogongwa," imesema ofisi hiyo.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskyy, anaishutumu Russia kwa vifo vya raia 300 katika mji ulio karibu na Kyiv, wakati akijiandaa kulihutubia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, jana.

Ikiwa ni siku ya 41 tangu Russia ianze mashambulizi nchini Ukraine, hasira inaendelea baada ya ugunduzi mkubwa wa miili mingi ya raia katika maeneo ambayo hapo awali yalikuwa chini ya udhibiti, karibu na mji wa Kyiv.

Nchi kadhaa za Ulaya zinawafukuza wanadiplomasia wa Russia, huku ghadhabu za kimataifa zikiongezeka, Moscow ikitarajiwa kujibu kwa hatua za papo hapo. Ufaransa imefungua uchunguzi kuhusu uhalifu wa kivita nchini Ukraine.

Meya wa Kyiv, amezitaka mamlaka za Ulaya kufuta uhusiano wa kibiashara na Russia, akidai shughuli za sasa zinafanywa kwa fedha za damu.

Hispania imewafukuza takriban wanadiplomasia 25 wa Russia na wafanyakazi wa ubalozi kutoka Madrid, Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo amesema.

Wakati huo huo, Marekani na washirika wake wanatarajia kutangaza vikwazo vipya vya kiuchumi dhidi ya Russia, huku Ukraine ikipokea msaada zaidi wa kijeshi.

Mshauri wa Usalama wa Kitaifa wa White House, Jake Sullivan, alitangaza hilo siku ya Jumatatu, wiki hii.

Hata hivyo Russia imekanusha kuhusika na mauaji hayo na imeomba mjadala katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ili kutoa uamuzi ikidai ni chuki zinazofanywa na Ukraine huko Bucha, kulingana na Moscow.

Vikosi vya Russia vinatayarisha shambulio kuwadhibiti wanajeshi wa Ukraine katika eneo la Lugansk Mashariki mwa Ukraine, gavana mkoa huo, Serguiï Gaïdaï, alitangaza.

Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz amesema kwamba Rais wa Russia Vladimir Putin na wafuasi wake watahisi athari na kwamba washirika wa magharibi wataimarisha vikwazo dhidi ya Moscow.

Wakati huo huo, mshauri wa masuala ya kiusalama wa Marekani Jake Sullivan alisema kuwa Marekani inafanya inashirikiana "kwa juhudi na washirika wake wa Ulaya kwa ajili ya kuweka vikwazo zaidi ili kuimarisha shinikizo na kuongeza gharama kwa Putin na kwa Urusi."

Ufaransa na Ujerumani pia zimesema kuwa zinaweza kuwafukuza mabalozi wa Urusi katika nchi zao.

Russia ilisema itajibu kwa kufunga milango ya balozi za Magharibi, Shirika la habari la Reuters iliripoti kuwa rais wa zamani wa Russia na Naibu Mkuu wa Baraza la Usalama Dmitry Medvedev alisema:

Itakuwa rahisi kwa kila mmoja. Halafu tutaishia kwa kutoangaliana kwa njia nyingine ila kwa njia ya mtutu wa bunduki," alionya.

UCHAGUZI MKUU KENYA 2022:

## Ruto: Kundi la watu wachache linasababisha maisha magumu

**Nairobi,** KENYA

NAIBU Rais wa Kenya, William Ruto, amedai kupanda kwa gharama ya maisha na uhaba wa mafuta nchini humo, kunasababishwa na watu wachache walioteka uchumi wa nchi hiyo.

Ruto amehoji, iweje bei ya mafuta nchini Kenya ni ghali ikilinganishwa na nchi jirani ilhali mafuta hayo yanapitia nchini humo, lakini akisema hali inayoshuhudiwa imesababishwa kimakusudi.

Hata hivyo, Ruto ameshtumiwa kwa kauli yake, kwa kile wakosoaji wake wanasema, yupo serikalini na anapaswa kuwajibika.

Kuna madai kwamba Naibu Rais William Ruto alinyimwa kuingia katika makazi yake rasmi mjini Mombasa kwa madai kwamba nyumba hiyo ilikuwa ikifanyiwa ukarabati.

Wakati wa uzinduzi wa ripoti ya BBI katika ukumbi wa Bomas of Kenya Novemba 2019, William Ruto, alizuiliwa katika mkutano kati ya Rais Uhuru Kenyatta na Raila, pia ilidaiwa kwamba msafara wa magari ya Ruto ulitakiwa kuondoka katika eneo hilo, baada ya Uhuru na Raila kuondoka.

Mwezi Agosti mwaka jana, naibu wa rais alizuiliwa kusafiri kwenda Uganda akiandamana na mwekezaji mmoja wa Uturuki, ambaye serikali inadai ni mfadhili wa ugaidi.

Mikutano ya kisiasa ambayo William Ruto alitarajiwa kuhudhuria pia ilifutiliwa mbali katika dakika za mwisho na mara nyingine maofisa wa polisi wametumia vitoa machozi kuwatawanya waliohudhuria. Wakati wa sherehe za siku ya madaraka iliofanyika mjini Kisumu, Rais alivunja itikafi ambayo imekuwepo kwa kumualika Raila Odinga na wazungumzaji wengine kuzungumza baada ya naibu wa rais kumualika rais kuzungumza na taifa.

Katika uongozi wa bunge, rais aliwaondoa viongozi wote wanaomuunga mkono naibu wa rais, akiwamo kiongozi wa wengi katika bunge la kitaifa na lile la seneti, viranja wa wengi katika mabunge yote hayo mbali na wanachama wa kamati tofauti bungeni.

**Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**

HABARI MICHEZO

# KIPA WA GENDARMERIE AMPA MANULA KIWANGO CHA ULAYA

Na Mwandishi Wetu

KIPA wa US Gendarmerie, Saidu Hamisu, aliyesimama langoni katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika wakati Simba ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0, amekunwa na kiwango cha Aishi Manula huku akimwombea mema apate nafasi kucheza soka Ulaya.

Manula ambaye amekuwa akionyesha kiwango cha juu kwenye michuano hiyo, ikiwa ni pamoja na kucheza penalti mbili katika mechi dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast iliyopigwa Benin, amekuwa gumzo kwenye mashindano hayo msimu huu.

Akizungumza baada ya mechi hiyo Jumapili iliyopita, Hamisu alisema kama akiambiwa achague mchezaji mmoja aliyeonyesha ubora zaidi kwenye mechi hiyo, atamchagua golikipa mwenzake wa Simba, Manula.

**"Nitamchagua kipa wa Simba [Aishi Manula] kwa sababu ni kipa bora, ninamwombea asonge mbele, ninamwombea aende Ulaya, ninamwombe kutafuta malisho mazuri zaidi, hata hapa Simba ni sehemu nzuri ila kila mmoja anaomba kusonga mbele.**

"Ninakuombea kupiga hatua mbele zaidi na kupata maendeleo ya kutoka hapa ulipo, ninakutakia mafanikio mema," alisema kipa huyo wa Gendarmerie, ambaye alikuwa chanzo cha Simba kupata bao la nne baada ya kushindwa kuuzuia mpira aliorudishiwa na beki wao.

Kwa matokeo hayo, Simba imetinga robo fainali ambapo katika droo iliyochezeshwa jana jijini Cairo, Misri yalipo Makao Makuu ya Shirikisho la Soka Afrika, imepangwa kukutana na Orlando Pirates ya Afrika Kusini ambapo itaanzia nyumbani Aprili 17, mwaka huu.

Katika hatua ya makundi, Simba ilimaliza nafasi ya pili ikiwa na pointi 10 sawa na vinara RS Berkane ya Morocco ambao waliwazidi kwa faida ya bao timu hizo zilipokutana (head to head).

Gendarmerie ambayo iliambulia alama tano pekee, imeburuza mkia katika Kundi hilo la D, wakati Asec Mimosas ikimaliza nafasi ya tatu ikiwa na pointi tisa.

TUTAKINUKISHA...




Kibu Denis (kushoto) na Clatous Chama wakiwa mazoezini jana kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union itakayopigwa keshokutwa, Alhamisi katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga. **PICHA: SIMBA**

## Beki Asukile apiga mbili akiibeba Prisons

Na Adam Fungamwango

BEKI wa Tanzania Prisons na nahodha wa timu hiyo, Benjamin Asukile, amesema kuwa zamani alikuwa akicheza kwenye nafasi ya ushambuliaji, hivyo ahikuwa ajabu sana kwake kucheza mbele juzi katika Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya dhidi ya Dodoma Jiji.

Asukile aliwashangaza wengi alipoingizwa kipindi cha pili na kufunga mabao mawili yaliyoipa ushindi wa 3-2 timu yake, ikiwa ni ushindi wa kwanza tangu kuanza kwa mwaka huu, pia ukiwa wa kwanza kwa Kocha Mkuu, Patrick Odhiambo tangu ajiunge kuinoa timu hiyo.

"Watu wengi hawajui kuwa zamani nilikuwa nacheza straika kabla sijaanza kucheza beki, sema nimeanza kujulikana nikiwa nacheza nafasi za nyuma, lakini naweza pia kucheza kama mshambuliaji, kocha aliniamini, nikasoma mchezo, nilipoingia nikaenda kusimama sehemu ambazo walikuwa na mapungufu, nikafunga mabao hayo na kuisaidia timu yangu," alisema nahodha huyo.

Kocha Mkenya, Odhiambo alisema aligundua Asukile ni mzuri pia akicheza mbele, baada ya kumuona kwenye mazoezi.

"Nilimwangalia kwenye mazoezi jinsi alivyokuwa akicheza kama straika na wenzake, nikaona ana kitu na anaweza kuwasaidia wenzake mbele, ndiyo maana nilipofanya mabadiliko, nikamwambia leo nenda kacheze kama straika na fanya kama unavyofanya kwenye mazoezi, na kweli ikawa hivyo," alisema.

Asukile aliingia wakati timu yake ikiwa nyuma kwa mabao 2-1, akapachika mabao mawili dakika ya 77 na dakika za majeruhi.

Umekuwa ni ushindi wa kwanza kwa Prisons tangu ilipoifunga Kagera Sugar bao 1-0 kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, Desemba 26, mwaka jana.

Baada ya hapo ilicheza mechi saba bila ushindi, ikipoteza nne na sare tatu. Matokeo hayo yameifanya kutoka mkiani na kupanda nafasi moja juu, ikiwa na pointi zake 19.

# *Mtibwa, Biashara zataka msaada kimataifa*

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Biashara United na Mtibwa Sugar zimeomba serikali isaidie gharama kwa timu ambazo zitashiriki michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho kutokana na kuwa kubwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, viongozi wa klabu hizo wamesema hayo kutokana na timu nne kuwa na uwezekano wa kupata nafasi ya kucheza michuano ya kimataifa mwakani baada ya Simba kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mwenyekiti wa Klabu ya Biashara United, Selemani Mataso, mbali na kuipongeza Simba kwa juhudi zake za kufanikisha kupeleka tena timu nne msimu ujao, ameiomba serikali kuzisaidia timu baadhi ya gharama ili ziweze kumudu kushiriki michuano hiyo.

"Timu kama Simba, Yanga na Azam zina uwezo wa kifedha, michuano hii ina gharama kubwa sana kuanzia kwenye usafiri, malazi na mambo mengine mengi, kwa hiyo tunaiomba serikali ambayo kwa sasa imeshaonyesha nia ya kutenga fedha kusaidia kwenye michezo, hasa timu za taifa, kufanya hivyo hata kwa klabu ambazo zinashiriki michuano ya kimataifa," alisema Mataso ambaye msimu huu timu yake ilishindwa kusafiri kwenda kucheza mechi ya Kombe la Shirikisho dhidi ya Al Ahly Tripoli ya Libya kwenye mechi ya raundi ya kwanza, ambapo ilishinda mabao 2-0 nyumbani, lakini ikashindwa kwenda ugenini, hivyo kutolewa kwenye michuano hiyo.

Thobisa Kifaru, Msemaji wa Mtibwa Sugar, yeye alisema baadhi ya timu za Tanzania hazina uwezo wa kifedha au bajeti za kuhimili gharama za michuano hiyo, hivyo mbali na timu yenyewe kujigharamia, lakini serikali inaombwa kugharamia japo usafiri tu kwa timu zake zinazocheza mechi za kimataifa, hasa zile ambazo hazijiwezi.

## ZISIKUPITE

### ERIKSEN LULU SPURS, UTD
KLABU ya zamani ya Christian Eriksen, Tottenham na Manchester United wanafikiria kumsajili kiungo huyo wa kati wa Denmark mwenye umri wa miaka 30, kwa uhamisho huru baada ya kurejea katika kiwango bora cha mchezo katika klabu ya Brentford. (***Mail***)

### SALAH SAFI LIVERPOOL
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema "anafurahi" na jinsi mazungumzo ya mkataba mpya yanavyoendelea na mshambuliaji, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29. (***Liverpool Echo***)

### MBAPPE KUMBADILI SALAH
BADO kuna matumaini kwamba Liverpool wanaweza kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, kutoka Paris St-Germain msimu huu - iwapo Salah ataamua kuondoka. (***FourFourTwo***)

### ABRAHAM KUREJEA EPL
MSHAMBULIAJI wa AS Roma, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 24, amedokeza uwezekano wa kurejea Ligi Kuu England, EPL. (***Talksport, via Mail***)

### ISAK NA USAJILI ARSENAL
MATUMAINI ya Arsenal kumsajili mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 22, yatapata msukumo mkubwa ikiwa Real Sociedad itashindwa kupata nafasi ya kucheza mashindano ya Ulaya msimu huu. (***Fichajes, via Football.London***)

### GNABRY KUONDOKA BAYERN
WINGA wa Ujerumani, Serge Gnabry mwenye umri wa miaka 26, anafikiria kuondoka Bayern Munich msimu huu wa majira ya joto huku Real Madrid na Liverpool zikiwania saini yake. (Goal)

### HAZARD KWA MKOPO
REAL Madrid wanatazamia kumtoa kwa mkopo winga wa Ubelgiji, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 31 kwa ajili ya kuanza kwa msimu wa 2022/23. (***AS***)

### HUBERS AGOMBEWA ENGLAND
TIMO Hubers wa FC Cologne analengwa kwa pauni milioni sita na Newcastle, Leeds na Crystal Palace msimu huu wa majira ya joto, huku West Ham, Southampton na Fulham pia wakimfuatilia beki huyo wa kati wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 25. (***Mail***)

### PHILLIPS MSHAHARA MKUBWA
KLABU ya Newcastle inaweza kumpa kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips mkataba wa kulipwa mshahara wa pauni 120,000 kwa wiki ili kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, kutoka kwa wapinzani wao wa Ligi Kuu, Leeds. (***Mirror***)

### NEVES AVUTIWA BARCA
KIUNGO wa kati wa Wolves, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25, anavutiwa na Barcelona, wakati mchezaji mwenzake wa Ureno, Joao Moutinho mwenye miaka 35, pia anaweza kuondoka hapo kwenye dimba la Molineux msimu wa majira ya joto. (***Athletic***)

### NEWCASTLE NA AWONIYI
NEWCASTLE wameambiwa pauni milioni 25 zitatosha kuwajaribu Union Berlin kumuuza mshambuliaji wa Nigeria, Taiwo Awoniyi msimu huu wa majira ya joto, ingawa West Ham na Southampton pia wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. (***Bild***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ROONEY: POGBA ANAPASWA KUONDOKA MANCHESTER UTD

## ●●● Pengine imefika wakati ambao ni bora kwake kusonga mbele ili...

**MANCHESTER,** ENGLAND

PAUL Pogba anapaswa kuondoka Manchester United mwishoni mwa msimu huu, kwa mujibu wa Wayne Rooney.

Pogba, mchezaji aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi pale United, alirejea Old Trafford mwaka 2016 baada ya kung'ara kule Juventus.

Nyota huyo wa Ufaransa hakupata nafasi United mapema katika maisha yake ya soka, lakini akawa mmoja wa viungo bora kule Turin.

Hata hivyo, hatua ya kurejea tena United imeshindwa kuleta mafanikio ambayo yalikuwa yametazamwa, huku United ikishinda mataji mawili pekee tangu Pogba asajiliwe.

Mustakabali wa Pogba umekuwa mjadala kwa muda mrefu, na kiwango cha Bruno Fernandes tangu kuwasili kwake Januari 2020, kimemweka kwenye hatari zaidi nafasi ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29.

**Mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na, hadi sasa hakuna makubaliano yoyote yaliyofanywa kuhusu mkataba mpya, na mchezaji mwenzake wa zamani wa Pogba, Rooney anafikiri wakati wake wa kuondoka umefika.**

Rooney aliiambia Sky Sports: "Pengine imefika wakati ambapo ni bora kwake kusonga mbele.

"Kama Paul angekuwa mwaminifu kwake mwenyewe labda hajapata matokeo ambayo angependa tangu aliporejea Manchester United.

"Ninamtazama akiichezea Ufaransa na ni mchezaji tofauti kabisa mwenye kila kitu, maono yake, udhibiti wake wa mchezo upo kila mechi kwa Ufaransa."

Rooney, mfungaji bora wa mabao wa United, pia alisisitiza kuwa sehemu ya tatizo ni ukosefu wa kocha aliyetulia wakati Pogba akiwa klabuni hapo.

"Hakujawa na kocha aliyetulia hapo tangu kuondoka kwa Alex Ferguson, kwa hiyo yeyote anayekuja anahitaji muda wa kujenga upya uhusiano na wachezaji hao," aliongeza.

"Ninaelewa kwamba (Ole Gunnar Solskjaer alikuwa mahali hapo kwa karibu miaka mitatu), lakini nadhani walikuwa wakipitia kipindi cha mpito na haikufanya kazi, na nadhani hiyo ni dhahiri kwa Ole, lakini nadhani mwishowe haijafanya kazi."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,119

MECHI KALI
CHELSEA
VERSUS
REAL MADRID
1 | 2.02
X | 3.31
2 | 3.67

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ARTETA AHOFIA NYOTA WAKE WAWILI ARSENAL

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema jeraha la goti la Kieran Tierney "halionekani zuri", ni wakati beki huyo akitarajia kuonana na mtaalam, huku Thomas Partey pia akiwa na wasiwasi kuhusu utimamu wa mwili wake.

Tierney aliichezea Scotland mara mbili wakati wa mapumziko ya kimataifa, lakini hakuwapo kwenye mchezo wakati 'Washikabunduki' hao walipofungwa mabao 3-0 na Crystal Palace, Jumatatu.

Baada ya kushindwa kule Selhurst Park, Arteta alithibitisha kuwa beki huyo wa kushoto alihisi tatizo ambalo litatathminiwa zaidi katika wiki hii, ingawa utabiri wa awali si mzuri.

"Alirudi kutoka kwenye majukumu ya kimataifa na akahisi kitu kibaya kwenye goti lake," alisema Arteta akiiambia BBC Sport.

"Kuna uharibifu huko. Tunatumaini tutajua zaidi Jumanne (jana), lakini haionekani vizuri.

"Anamwona mtaalamu Jumanne (jana) na tutajua zaidi kuhusu ukubwa wa jeraha, lakini hisia aliyokuwa nayo haikuwa nzuri na kila uchunguzi ulionyesha pia. Tunapaswa kusubiri na kuona kitakachotokea."

Arsenal wanaweza kupoteza mchezaji mwingine muhimu kutokana na jeraha walipokuwa wakielekea katika mchezo wa pili, huku Partey akitoka nje akiwa na jeraha la misuli ya paja.

## Madrid hawamuuzi tena Hazard

**MADRID,** Hispania

REAL Real Madrid imebadili mawazo kwa mchezaji wao nyota, Eden Hazard kuhusu hatma yake kwenye klabu hiyo baada ya awali kupanga kumuweka sokoni kwa kutaka kumuuza moja kwa moja.

Hazard hana msimu mzuri kwenye klabu hiyo tangu aliposajiliwa kwa kitita kikubwa akitokea Klabu ya Chelsea mwaka 2019, huku akiwa anapambana kuweza kurejesha kiwango chake na majeraha ya mara kwa mara.

Hata alipokuwa sawa kiafya kocha Carlo Ancelotti amekuwa akiwapa nafasi zaidi Marco Asensio na Rodrygo, na hata anapopata nafasi kwenye kikosi cha Real Madrid bado amekuwa hana kiwango kizuri.

Kwa sasa Hazard yuko nje ya kikosi cha Real Madrid anafanyiwa upasuaji wa pili ili kuweza kuondoa kifaa alichowekewa alipovunjika mfupa mwaka jana, na atakosekana kwenye kikosi cha 'Los Blancos' kwa wiki sita.

Madrid kwa sasa wamefuta mpango wao wa kutaka kumuuza, bali wanahitaji kumpeleka kwa mkopo wa muda mrefu ili aweze kupata nafasi zaidi ya kucheza.

Klabu ambayo itahitaji kumchukua kwa mkopo itabidi wakubali kuchangia mshahara wake.



,012,860

# DAKTARI ASHINDA MILIONI 49/- JACKPOT BONUS YA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Buhongwa wilayani Nyamagana jijini Mwanza, Anicet Clavery Macheta, ameshinda shilingi 49,041,581 kwenye Jackpot Bonasi ya Sportpesa iliyochezwa mwishoni mwa wiki iliyoisha, baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya 13.

Akizungumza baada ya makabidhiano ya mfano wa hundi katika Ofisi za Sportpesa jijini Dar es Salaam, Anicet alisema alianza kucheza na Sportpesa tangu mwaka 2018, baada ya kuona matangazo na wachezaji wengine wakishinda.

"Mimi ni mpenzi wa mchezo wa mpira, hivyo wakati bado ni mwanafunzi wa udaktari pale Muhimbili, siku moja wakati tunaangalia mpira alitokea kijana mmoja ameshika karatasi anashangilia kwa furaha. Nilipomuuliza vipi mwenzetu akasema ameshinda fedha kwenye mechi tulizotoka kuangalia," alisema.

Anicet alisema kitendo cha kijana huyo kushinda kilimvutia kumuuliza maswali zaidi namna ya kucheza, hivyo baada ya hapo alianza rasmi kucheza.

"Nilifuatilia namna ambavyo nilisikia kwa vijana wenzangu na kugundua kupitia 'sms' (ujumbe mfupi wa maneno) na mitandao matokeo ya Jackpot yalikuwa yanaonyesha viwango vya ushindi kwa waliopata mechi 10, 11 na 12, hilo lilinishawishi kuanza kucheza nao."

Akielezea namna alivyopata ushindi huu wa Jackpot Bonasi, alisema aliweka mkeka wake Ijumaa baada ya kuichambua na kufanyia utafiti mechi kwa siku zaidi ya tatu.

"Staili yangu mimi huwa siweki mikeka mingi ya Jackpot. Huwa naweka mkeka mmoja kwa dau lililoshiba kama ishara ya kujiamini, nikicheza zaidi dabo 'kombinesheni'," alifafanua.


Alisema baada ya hapo Jumamosi hakufuatilia mechi kwa kuziangalia moja kwa moja ila aliende mazoezini kukimbia ili aondoe hofu ya kupoteza ushindi wa mikeka yake.

"Nilimaliza mazoezi muda ambao mechi zilikuwa zimeisha na nilipocheki matokeo nikakuta nimepatia timu tisa kati ya 10 za siku hiyo."

Anicet alisema kuwa Jumapili nayo ilikuwa ngumu kidogo kwani kila alipofikiria mikeka yake alipata shauku na hofu kwa kuwa zilikuwa zimebaki mechi chache, hivyo muda wa mechi ulipofika alijipa shughuli iliyomweka mbali na taarifa za matokeo ya mechi zilizosalia.

"Baada ya zile mechi kuisha niliendа kufungua kompyuta yangu na kuangalia matokeo mnamo majira ya saa 1:05 usiku. Nilikuta nimeshinda mechi 12 kati ya 13 na hivyo kupata sms ya ushindi wa bonasi ya timu 12 dakika tano baadaye.

Kutoka Sportpesa, Meneja Uhusiano na Mawasiliano, Sabrina Msuya, aliongeza kwa kuwahamasisha Watanzania kucheza Jackpot ya Sportpesa hasa katika kipindi hiki ambapo ligi mbalimbali zimerudi kama EPL, Championship, LaLiga na Bundesliga ili kujishindia zawadi mbalimbali kama 20,000 kila siku, mmilioni moja kila wiki na Aprili 12, mwaka huu zawadi kubwa ya shilingi 15,888,000 zitatolewa kwa mshindi wa kufungia promosheni hii.




Mshindi wa SportPesa Jackpot Bonasi, Ancent Macheta (wapili kulia) kutoka Mwanza akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 49 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot inayoshindaniwa wiki hii ni Sh. 1,119,012,860. Miongoni mwa walioshuhudia makabidhiano hayo ni pamoja na wachezaji wa Simba, kutoka kushoto Meddie Kagere, Pape Sakho na Shomari Kapombe (kulia). **MPIGAPICHA WETU**

# Simba sasa akili zote Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema inaachana na shamrashamra za kutinga robo fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, na sasa mawazo yake inayaelekeza kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union keshokutwa, Alhamisi.

Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemanu, amesema kwa sasa hawaizungumzii tena robo fainali ya michuano hiyo ya Afrika, bali wanaangalia jukumu lililo mbele yao la kucheza mechi ya ligi dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

"Tumeweza kupata matokeo bora yaliyotarajiwa, tunashukuru wachezaj na mashabiki ambao kusema kweli walitupa sapoti kubwa, lakini kwa sasa hatuizungumzii tena mechi hiyo wala kuendelea na shamrashamra, lakini tuna jukumu tarehe saba dhidi ya Coastal Union.

"Tunashiriki michuano ya kimataifa kwa sababu ya kucheza ligi ya ndani, kwa hiyo lazima nayo tuipe heshima yake, haitakuwa mechi nyepesi, tunaiheshimu Coastal Union kwa sababu tulitoka nao suluhu mechi ya mzunguko wa kwanza na tuna ratiba ngumu sana kwani baada ya tarehe saba, kuna mechi tarehe kumi na 13," alisema meneja huyo.

Alisema wachezaji wa timu hiyo baada ya mechi dhidi ya US Gendamarie Jumapili iliyopita, waliendelea na mazoezi kesho yake jioni kwa ajili ya kuendelea na ligi, huku mchezaji Mohamed Hussein 'Tshabalala', ambaye aliumia kwenye mechi hiyo akiwa chini ya uangalizi wa madaktari, lakini hali yake ikiendelea vizuri.

"Tatizo lilikuwa ni misuli si kingine, lakini hali haikuwa mbaya sana, alifanyiwa vipimo, hivi sasa yupo chini ya uangalizi wa madaktari, lakini hali yake ni nzuri na anaweza kucheza kwenye mechi ijayo," alisema Rweyemamu.

Alisema kwa sasa wanashukuru Mungu kwani wamebakiwa na majeruhi mmoja tu ambaye ni Hassan Dilunga, na kwamba waliobaki wote wako fiti kuivaa Coastal.


# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/04/22 | 17:00 | Watford vs Leeds | 2.75 | 3.29 | 2.49 |
| 02. 09/04/22 | 17:00 | Preston vs QPR | 2.48 | 3.17 | 2.77 |
| 03. 09/04/22 | 17:00 | Bolton vs Sheffield Wed | 2.63 | 3.13 | 2.63 |
| 04. 09/04/22 | 19:30 | Hertha BSC vs Union Berlin | 2.69 | 3.19 | 2.59 |
| 05. 09/04/22 | 20:00 | Amiens vs Bastia | 2.63 | 2.93 | 2.78 |
| 06. 10/04/22 | 15:15 | Servette Geneva vs FC Zurich | 2.37 | 3.48 | 2.73 |
| 07. 10/04/22 | 16:00 | Sivasspor vs Basaksehir | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 08. 10/04/22 | 16:00 | Brentford vs West Ham | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 10/04/22 | 16:00 | Norwich City vs Burnley | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 10. 10/04/22 | 16:00 | Brest vs Nantes | 2.43 | 3.22 | 2.92 |
| 11. 10/04/22 | 17:15 | Espanyol vs Celta Vigo | 2.78 | 3.13 | 2.63 |
| 12. 10/04/22 | 17:30 | St. Gallen vs FC Basel | 2.39 | 3.53 | 2.68 |
| 13. 10/04/22 | 20:00 | Strasbourg vs Lyon | 2.60 | 3.30 | 2.65 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 06/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 5496 | Urawa Red Diamonds vs Shimizu S Pulse | 1.74 | 3.36 | 4.38 |
| 14:00 | 4992 | Lusaka Dynamos vs Kabwe Warriors | 1.39 | 3.90 | 7.99 |
| 14:05 | 5911 | Perth Glory vs Melbourne Victory | 4.07 | 3.67 | 1.80 |
| 15:00 | 3859 | Parma vs Como | 1.60 | 3.71 | 5.35 |
| 15:00 | 5030 | Yenisey Kr vs Gazovik Orenburg | 3.30 | 3.30 | 2.02 |
| 15:00 | 5630 | Fasil Kenema vs Wolkite City FC | 1.52 | 3.70 | 5.84 |
| 15:00 | 5657 | FC Krasnodar II vs Neftekhimik | 3.31 | 3.31 | 2.02 |
| 16:00 | 1130 | Power Dynamos vs Chambishi FC | 1.54 | 3.31 | 6.81 |
| 16:00 | 1160 | Spartak II Moscow vs Fakel | 3.99 | 3.41 | 1.80 |
| 16:00 | 1429 | FC Olimp Dolgoprudny vs Volgar Astrahan | 2.39 | 2.91 | 2.96 |
| 16:00 | 2366 | Konkola Blades vs Green Buffaloes | 3.66 | 2.68 | 2.20 |
| 16:00 | 2753 | Buildcon vs Indeni FC | 1.87 | 3.07 | 4.19 |
| 16:00 | 2810 | Forest Rangers vs Zesco United | 3.42 | 2.79 | 2.23 |
| 16:00 | 3382 | Dove All Stars vs Gaddafi FC | 2.15 | 3.01 | 3.30 |
| 16:00 | 3512 | Biashara United vs Mbeya Kwanza FC | 1.39 | 3.90 | 7.99 |
| 16:00 | 4152 | Green Eagles vs Nkana FC | 2.09 | 2.86 | 3.69 |
| 16:00 | 4496 | Prison Leopards vs Kansanshi Dynamos | 2.25 | 2.62 | 3.64 |
| 16:00 | 5146 | Nkwazi vs Red Arrows | 2.77 | 2.57 | 2.86 |
| 17:00 | 1062 | EN Paralimni vs Ethnikos Achnas | 3.15 | 3.30 | 2.24 |
| 17:30 | 5998 | Dukla Prague vs Jihlava | 1.72 | 3.45 | 4.37 |
| 17:35 | 3472 | Real Kashmir vs Churchill Brothers | 2.72 | 3.16 | 2.41 |
| 18:00 | 1219 | Tekstilshchik vs Metalurg Lypetsk | 2.29 | 3.01 | 3.01 |
| 18:00 | 1781 | Bloemfontein Celtic vs Tshakhuma | 1.53 | 3.67 | 6.55 |
| 18:00 | 2668 | Golden Arrows vs Stellenbosch | 2.18 | 2.97 | 3.52 |
| 18:00 | 3786 | Baroka FC vs Amazulu | 2.82 | 2.62 | 2.92 |
| 18:00 | 5703 | KamAZ vs FC Rotor Volgograd | 2.52 | 3.00 | 2.71 |
| 18:30 | 4891 | Sekhukhune United vs Orlando Pirates | 3.57 | 2.47 | 2.53 |
| 19:00 | 2072 | Torpedo Moscow vs Akron Tolyatti | 1.40 | 4.08 | 7.18 |
| 19:00 | 2635 | Veles vs Ska Energiya | 2.97 | 2.97 | 2.35 |
| 19:00 | 3346 | Rostov vs Kryliya Sovetov | 2.73 | 3.07 | 2.58 |
| 19:00 | 3588 | Urozhay Krasnodar vs Tom Tomsk | 1.79 | 3.36 | 4.09 |
| 19:00 | 3607 | Anorthosis Famagusta vs Apoel Nicosia | 2.21 | 2.86 | 3.35 |
| 19:00 | 4932 | Molde vs Stromsgodset | 1.37 | 4.76 | 6.22 |
| 19:00 | 5337 | Rakow Czestochowa vs Legia Warszawa | 1.99 | 3.25 | 3.45 |
| 19:30 | 1493 | Augsburg vs Mainz | 3.20 | 3.25 | 2.22 |
| 20:00 | 3328 | Vicenza vs Crotone | 2.12 | 3.32 | 3.27 |
| 20:00 | 3618 | Pisa vs Brescia | 2.53 | 3.02 | 2.83 |
| 20:00 | 5611 | Monza vs Ascoli | 1.53 | 3.97 | 5.76 |
| 20:00 | 5992 | Cittadella vs Perugia | 2.54 | 2.99 | 2.84 |
| 20:30 | 2155 | Moroka Swallows FC vs Mamelodi Sundowns | 5.56 | 2.88 | 1.81 |
| 20:30 | 4061 | Maritzburg Utd vs Cape Town City | 2.26 | 2.97 | 3.32 |
| 21:30 | 1921 | Burnley vs Everton | 2.49 | 3.09 | 2.89 |
| 21:45 | 4133 | Dunfermline vs Raith Rovers | 2.18 | 3.35 | 3.05 |
| 21:45 | 4823 | Nottingham vs Coventry | 2.03 | 3.37 | 3.42 |
| 21:45 | 5682 | Middlesbrough vs Fulham | 3.17 | 3.32 | 2.16 |
| 22:00 | 2404 | West Bromwich vs Bournemouth | 2.52 | 3.17 | 2.72 |
| 22:00 | 4012 | Villarreal vs Bayern Munchen | 4.98 | 4.28 | 1.57 |
| 22:00 | 5222 | Chelsea vs Real Madrid | 2.02 | 3.31 | 3.67 |
| 22:30 | 1240 | Pyramids vs Zamalek | 2.06 | 3.18 | 3.62 |
| 22:30 | 5429 | Al Ahly Cairo vs El Ittihad Alexandria | 1.22 | 5.77 | 11.93 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatano Aprili 6 , 2022
Nipashe



'Pogba anapaswa kuondoka Man U'
UKURASA 21

WANATOKAJE?...



Wachezaji wa Yanga wakiwa mazoezini kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Azam FC, itakayopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi leo usiku. **PICHA: YANGA**

## Azam, Yanga 'hatoki mtu' Chamazi leo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Yanga ikidhamiria kuondoka na alama zote tatu leo dhidi ya Azam FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, wenyeji wao hao wamesema haitakuwa rahisi kwa kila upande.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alimwambia mwandishi wetu kuwa mechi hiyo ni kama fainali, huku Ofisa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli akisema lengo lao ni kuhakikisha msimu huu Azam FC inawapa alama zote sita.

Yanga ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 48, iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 timu hizo zilipokutana mzunguko wa kwanza Oktoba 30, mwaka jana, hivyo kama vinara hao watashinda leo, Azam itakuwa miongoni mwa timu zilizoipa pointi zote sita msimu huu.

Kaze aliliambia gazeti hili kuwa itakuwa mechi ya ushindani mkubwa kwa sababu timu zote zinajuana, lakini wataingia kivingine kutafuta alama tatu.

"Azam FC watakuwa nyumbani katika uwanja wao waliouzoea, lakini tutawakabili kwa nidhamu na mbinu tofauti ili kuweza kupata matokeo chanya," alisema Kaze.

Kwa upande wa Bumbuli, alisema hawapendi kuongea sana, lakini timu yao imefanya maandalizi ya kutosha kuweza kuvuna pointi tatu kama walivyofanya mzunguko wa kwanza.

Hata hivyo, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Azam FC, Zakaria Thabit 'Zaka Zakazi', alisema wanakwenda kucheza na Yanga ambao wapo katika kiwango kizuri sana msimu huu wakiwa pia na wachezaji wazuri na bahati ikiwaangukia pia msimu huu, lakini hiyo haiwezi kuwa sababu ya wao kushindwa kupata matokeo.

"Wanasema wana majeruhi [Khalid] Aucho na Fei Toto [Feisal Salum], lakini bado wana Sure Boy [Salum Abubakar], ambaye ni mchezaji mzuri na alifanya mambo makubwa sana akiwa Azam FC, hivyo bado wana timu imara," alisema Zaka Zakazi wakati huu wakiwa nafasi ya tatu na alama zao 28.

# Simba: Tunaiona fainali CAF

### ●●● Kuivaa Orlando Pirates ya Sauzi robo fainali, ikipenya kwa Waarabu wa Libya, yatamba...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeonyesha kufurahia droo ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), iliyopangwa Cairo nchini Misri jana alasiri, ikionyesha itacheza dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika ya Kusini Aprili 17, kwa kuanzia Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kabla ya mechi ya marudiano ugenini Aprili 24, mwaka huu.

**Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema baada ya droo hiyo kuwa wanaiona fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho iko jirani, kwani itakwenda kucheza na timu ambayo ni saizi yao, inayotoka chini ya Jangwa la Sahara kama wao.**

Pia ameongeza kwamba itakuwa ni mechi ya kufuta kumbukumbu ya kutolewa dhidi ya Kaizer Chiefs msimu uliopita ambapo ilifungwa mabao 4-0 nchini Afrika Kusini, kabla ya kushinda 3-0 nchini, lakini hayakutosha kuwafanya waendelee.

"Tumefurahi kucheza na Orlando Pirates kwa sababu ni mpinzani ambaye ni saizi yetu na tunammudu, wote tunatoka chini ya Jangwa la Sahara, na tunataka kufuta kumbukumbu ya kutolewa msimu uliopita, ingawa hatukutolewa nao, lakini tulitolewa na jirani zao Kaizer Chiefs, sasa tunataka tuuzime msimu huo, na baada ya hapo inaonyesha kuwa tutatacheza na mshindi kati ya Al-Ittihad dhidi ya Al Ahly Tripoli za Libya, kwa hapa naiona kabisa fainali kwa Simba," alisema Ahmed.

Alisema kwa sasa wanapaswa kupiga hesabu kali kwani kwenye michuano hii ya Afrika, mara nyingi timu hushinda nyumbani, hivyo watakwenda kujipanga kushinda mabao mengi nyumbani na hata kushinda ugenini, au kutoruhusu mabao.

"Tunajua tuna matatizo ya kutoshinda au kufanya vibaya mechi za ugenini, lakini tumejifunza mengi kuwa kwenye michuano hii, timu inatakiwa ifunge mabao mengi nyumbani, pia iwe na uwezo wa kushinda ugenini, au kutoruhusu mabao mengi, hilo tunakwenda kulirekebisha," alisema.

Naye mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Simba Mulamu Ng'ambi mbali na kusema kuwa mechi hiyo ni kama marudio tu ya mechi ya Ligi ya Mabingwa msimu uliopita Mei mwaka jana, lakini wao kama Simba watakaa na kuona wanatokaje hatua ya robo fainali ambayo huwa wanakomea mara kwa mara na kwenda nusu fainali.

"Kwa misimu minne sasa, tumeingia robo fainali mara tatu kwenye michuano ya kimataifa, mara mbili tumetolewa, sasa ni wakati wa kwenda mbele zaidi ya hapo. Tumejifunza mengi kwenye michuano hii, ni kwamba unatakiwa kutumia nafasi unazozipata unapocheza nyumbani na kupata ushindi mzuri, na kama tukipita hapa kuna uwezekano na kwenda fainali," alisema Mulamu.

Orlando Pirates ilimaliza kinara kwenye Kundi B ikiwa na pointi 13, ikishinda mechi nne, sare moja na kufungwa moja.

Kwenye mechi sita ilizocheza, imeshinda mbili ugenini mabao 6-2 dhidi ya Royal Leopards ya Eswatini na 2-0 dhidi ya JS Saoura ya Algeria, huku mechi pekee iliyopoteza ni dhidi ya Al-Ittihad ya Libya kwa mabao 3-2 ikicheza ugenini, lakini ikatoka suluhu nyumbani dhidi ya timu hiyo hiyo kwenye mechi ya mwisho ya kundi hilo.

Kwenye michuano hiyo, Pyramids ya Misri itacheza robo fainali yake dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya DR Congo, huku Al-Ittihad ikicheza na Walibya wenzao, Al Ahly Tripoli, wakati Al Masry ya Misri ikiivaana na RS Berkane ya Morocco. Mshindi kati ya TP Mazembe na Pyramids atacheza nusu fainali na mshindi kati ya Al Masry na RS Berkane.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >